
# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 4 | Septemba 25, 2022 JARIDA LA JUMAPILI BILA MALIPO

# AZIMIO INAZIMIA?

**Kuna dalili za Uhuru na Raila kutengana baada ya kushindwa vibaya katika uchaguzi mkuu wa Agosti 9. Kwa miaka mingi, Raila amekuwa kigogo wa siasa katika historia ya taifa, lakini huenda mwisho wake umewadia. Baada ya Uhuru kuondoka mamlakani, na huku Chama cha Jubilee kikipanga kujiondoa, muungano wa Azimio la Umoja unachungulia kaburi lake**

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*


# anywhere, anytime.

Follow the link to subscribe
> ***epaper.nation.africa.***

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play




Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111
Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

# Tunahitaji upinzani wenye nguvu kumulika serikali



Washington Gikunju

Mamilioni ya Wakenya waliopigia kura wagombea waliowapenda, na hata ambao hawakupiga, wanasubiri kwa hamu kutimizwa kwa ahadi nyingi zilizotolewa wakati wa kampeni.

Wabunge waliochaguliwa kwa tikiti ya Muungano wa Kenya Kwanza wa Rais William Ruto tayari wameelezwa ajenda ya sheria ya chama tawala, na kwa upande mwingine, wale wa Muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya wanajitayarisha kuwa upinzani katika Bunge la Kitaifa na mabunge ya kaunti kote nchini. Upinzani unafaa kutekeleza jukumu lake kwa shauku na kujitolea kupiga darubini Serikali Kuu na Mahakama. Hasara ni kwa nchi upinzani ukiwa dhaifu, kwa kuwa hakuna wa kuzuia maovu ya walio mamlakani.

Muhula wa pili wa serikali ya Jubilee ni mfanowa hali hiyo, Serikali Kuu ilipokosa wa kuikosoa kufuatia 'handisheki' kati ya upinzani na serikali.

Hatua zilizoumiza wengi kama kuongezwa kwa ushuru wa mafuta zilipita bungeni kwa urahisi, na kufanya gharama ya maisha kupanda.

Ilikuwa furaha kwa ndugu wawili wa 'handisheki' kwani kila kitu Serikali Kuu ilichotaka kilifanywa.

Kwa miaka mitano, nchi ilikuwa

**Uchumi wetu uko katika hali mbaya hivi kwamba ushindani wa kisiasa ni muhimu ili wapiga kura waweze kupata thamani kamili ya pesa zao. Matumizi mabaya kwa miradi isiyo na faida, au ufujaji usiothibitiwa kupitia ufisadi, yanaweza kufanya uchumi dhaifu kuporomoka.**

sawa na ilivyokuwa enzi za utawala wa chama kimoja, wakati hakuna aliyeweza kukosoa serikali kwa maovu yake. Ushirikishi wa umma inavyohitaji Katiba haukuzingatiwa ipasavyo. Ukweli ni kuwa, ingawa serikali na wanasiasa wanaweza kuwa na nia nzuri, hakuna kundi la watu au chama kinachoweza kuwa ndicho chenye mawazo mazuri. Upinzani chanya na ukosoaji, hata katika familia, huwa unaleta matokeo bora.

Uchumi wetu uko katika hali mbaya hivi kwamba ushindani wa kisiasa ni muhimu ili wapiga kura waweze kupata thamani kamili ya pesa zao.

Matumizi mabaya kwa miradi isiyo na faida, au ufujaji usiothibitiwa kupitia ufisadi, yanaweza kufanya uchumi dhaifu kuporomoka. Baadhi ya ahadi za kisiasa ni za kufurahisha na zisizoweza kutekelezwa kabisa, na upinzani unafaa kuzichunguza na kuzizima zikiwasilishwa bungeni kuhalalishwa kupitia sheria.

Kwa mfano, ahadi ya Hazina ya Mahasla ya Sh50 bilioni, wazo nzuri linaloweza kubadilisha maisha ya wafanyabiashara wengi wadogo, inaweza kugeuka kuwa kisima cha kunufaisha wakubwa wafisadi, kama ilivyotokea kwa Hazina ya Vijana. Mpango wa kuongeza ada za NSSF na NHIF pia unafaa kuchunguzwa kwa makini, ikizingatiwa kuwa wafanyakazi wa Kenya wamekuwa wakiteseka mikononi mwa mameneja wafisadi wakishirikiana na wafadhili wao, wanasiasa.

Muungano wa Azimio unafaa kutekeleza jukumu la upinzani na kuwa upande wa Wanjiku ili kuhakikisha serikali inatimiza ahadi ilizotoa wakati wa kampeni kwa gharama ya chini. Miswada mibaya inayokandamiza uhuru haifai kupitishwa kuwa sheria. Katika demokrasia, upinzani huwa serikali inayosubiri kuingia mamlakani. Miaka mitano ni sawa na kufumba na kufumbua jicho tu. Kando na kujenga nchi bora kwa wote, utendakazi mzuri katika upinzani unaweza kuzaa mazuri katika uchaguzi mkuu wa 2027.

*wgikunju@ke.nationmedia.com*

*Imetafsiriwa na Benson Matheka*

# Yaliyomo

8 **RAIS ALIVYODHIBITI MAMLAKA:** Ruto alichukua hatua haraka kuwinda wabunge na maseneta waliochaguliwa kwa tikiti ya vyama tanzu vya Muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya ili kuongeza idadi ya wale wa mrengo wake.

9 **MWANAMKE 'ALIYEMPIKA MAMBA':** Gavana wa Meru Kawira Mwangaza si mwanasiasa aliyetarajiwa kushinda wanasiasa wawili matajiri na wenye uzoefu wa miaka mingi kama Murungi na Linturi.

10 **UKWELI KUHUSU UCHUMI:** Kujenga uchumi wa nchi unaodorora kwa kutumia mfumo wa 'Bottom Up' kunahitaji mawazo mapya, ukuaji ukiwa ukipewa kipaumbele ndipo uweze kuleta faida na ajira.



11 **SI UREMBO TU, PIA NIA:** Polisi wa kike Emma Brenda Wanjiru hutumia mitandao yake ya kijamii kuzungumzia hali ya kuwa mwanamke mzazi asiye na mume, mimba za matineja na dhuluma za jinsia.

*Zimetafsiriwa na Benson Matheka*

Darubini Ya Wiki
Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Mutuma Mathiu** Mhariri Mkuu

**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji

**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Benjamin Situma, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

## Ubora wa filamu ya 'James Bond' kuendelea



Bendi ya kijeshi ikicheza kwenye zulia jekundu kabla ya kuzinduliwa kwa filamu ya James Bond *No Time to Die* katika ukumbi wa Royal Albert, magharibi mwa jiji la London, mnamo Septemba 28, 2021. PICHA I AFP

# Studio mpya ya 007 kuhudumia wote

Filamu ijayo ya James Bond itakuwa na ubora wa kipekee, amesema produsa Barbara Broccoli.

Hata hivyo, mazungumzo kati ya maprodusa na mmiliki mpya wa Studio 007 kuhusu mwelekeo mpya wa filamu hiyo bado hayajaanza. Broccoli na ndugu yake, Michael G Wilson, walisifiwa sana katika

Ukumbi wa Maigizo wa TCL Chinese Theatre, Hollywood, kwa mchango wao katika msururu wa filamu hiyo. Kufikia sasa, filamu hiyo ina jumla ya sehemu 25.

Filamu ya mwisho ya msururu wa James Bond ilikuwa "No Time To Die", iliyotolewa mwaka uliopita chini ya mwelekezi Daniel Craig, aliyemiliki studio hiyo wakati huo.

Hata hivyo, huenda mwelekeo ukawa tofauti, baada ya kampuni ya Amazon kuinunua. "Ndio tunaanza uhusiano wetu mpya na Amazon. Hatujaanza mazungumzo kuhusu mradi unaofuata wa filamu ya James Bond," akasema Brocolli. Hata hivyo, alisema watahakikisha filamu hiyo itakuwa bora zaidi.

## Aliyekuwa rais ashtakiwa kwa ulaghai

# Trump 'aliongezea utajiri wake'

Aliyekuwa rais wa Amerika, Donald Trump, ameshtakiwa katika mahakama moja jijini New York, kufuatia uchunguzi uliofanywa katika kampuni ya familia yake - Trump Organization.


Trump ameshtakiwa kwa kutoa maelezo ya uongo kuhusu kiwango halisi cha utajiri wake, ili kupata mikopo na kulipa kiwango cha chini cha ushuru.

Viongozi wa mashtaka wanasema kampuni hiyo ilitoa maelezo ya uongo kati ya 2011 na 2021. Hata hivyo, Trump amepuuzilia mbali mashtaka hayo akisema ni njama ya kuendelea kumhangaisha.

Wanawe Trump, Donald Junior, Ivanka na Eric Trump; na wasimamizi wawili wakuu wa kampuni hiyo, pia ni washtakiwa.

Wasimamizi hao ni Allen Weisselberg na Jeffrey McConney. Kesi hiyo imewasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa New York, Leitita James.

Uchunguzi huo ulifanywa kwa miaka mitatu. "Kupitia usaidizi wa wanawe na wasimamizi wakuu wa kampuni hiyo, Trump aliongeza utajiri wake ili kupata mikopo na kukwepa kulipa ushuru unaostahili," akasema mwanasheria huyo.



Rais wa Amerika Donald Trump (katikati), bintiye Ivanka Trump na mwanawe Donald Trump Jr. wakielekea kuabiri ndege ya Air Force One mjini Marietta, Georgia, mnamo Januari 4, 2021. PICHA I AFP

## Wakazi wakimbilia usalama kabla giza kuingia

# Mji watekwa na magenge ya wahalifu



Mji wa bandari wa Buenaventura, nchini Colombia, umegeuka uwanja wa uhalifu, kutokana na ongezeko la magenge ya wahalifu.
Visa ya uhalifu vinaipotiwa karibu kila siku, vikihusisha mivutano baina ya magenge hatari, baadhi yakiendesha biashara ya mihadarati. Kufikia saa sita adhuhuri, maduka huwa yamepunguza shughuli zake huku barabara nyingi zikiwa bila mtu yeyote. Watu wengi hukimbilia usalama wao kabla ya giza kuingia.

"Tunakabiliwa na wimbi jipya la uhalifu ambalo ni sawa na ugaidi mjini humu," akasema Juan Manuel Torres kutoka Hazina ya Amani na Maridhiano ya Colombia akihojiwa na AFP.

## Wacheza kamari walaghaiwa pesa

# Twitch yazima mchezo wa kamari




Tovuti ya Twitch imepiga marufuku majukwaa ambayo wachezaji kamari hucheza michezo ya moja kwa moja ambayo haijahalalishwa Uamuzi huo unafuatia kisa ambapo mchezaji kamari aliwapunja wachezaji wengine pesa zao bila wao kujua. "Suala la uchezaji kamari limekuwa likijadiliwa kwa upana. Tumepiga marufuku majukwaa hayo kuanzia Oktoba 18 kama njia ya kulainisha na kudhibiti oparesheni zetu," ikaeleza tovuti hiyo.

*- Zimetafsiriwa na Wanderi Kamau*


ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

HALI SI SHWARI TENA

# DHORUBA NDANI YA AZIMIO

*Huenda "ndugu wawili wa kisiasa" ambao vyama vyao viliunda muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya, wanavuta pande tofauti baada ya uchaguzi ulioibua ushindani mkali. Je, huu ni mwanzo wa kifo cha muungano huo?*



Kiongozi wa Azimio la Umoja Raila Odinga (kulia) na aliyekuwa mgombea mwenza wa urais, Martha Karua, mnamo Agosti 6.

Na OSCAR OBONYO

BAADA ya kukubali kundwa katika uchaguzi wa mwezi jana, hatimaye muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya umeamua kutekeleza wajibu wake kama upinzani.

Lakini maswali yameibuka kuhusu ni nani hasa atakuwa kiongozi wa muungano huo unapotekeleza wajibu wake wa kuhakiki utendakazi wa serikali ya Rais William Ruto.

Baada ya Uhuru Kenyatta kuondoka na Raila Odinga kushindwa na Ruto, haijulikani iwapo vinara hao wawili watataka kuendelea kuwa sura ya Azimio sasa na kuelekea 2027. Haijulikani pia iwapo wataamua kumkuza mwanasiasa mwingine kupeperusha bendera ya muungano huo.

Jarida la Darubini ya Wiki limegundua kuwa kiongozi wa Wiper, Kalonzo Musyoka, ameanza kujiandaa kwa kampeni za urais ili akabiliane na Rais Ruto katika uchaguzi mkuu wa 2027.

Karibu naye, ni Martha Karua, mgombea mwenza wa Raila, ambaye pia anasubiri wakati wake.

Pia kuna Katibu Mkuu wa Jubilee, Jeremiah Kioni, ambaye sasa anawakilisha sura ya chama hicho kinachoongozwa na Uhuru.

Chama hicho kimedumisha kundi na wapanga mikakati wake ili wakisaidie kujipanga upya na kuhakiki serikali ya Ruto.

Mikakati hii tofauti tayari inaonyesha viongozi wa Azimio wameamua kufuata mikondo tofauti ya kisiasa, kivyao.

Ukweli huu unathibitishwa na kauli aliyotoa Mbunge wa Saboti, Caleb Amisi, mapema wiki hii, akidai kuwa Raila bado atakuwa kwenye debe 2027.

Ingawa hii ni kauli ya kibinafsi ya mbunge huyo, huenda inawakilisha hisia za wanachama wengi wa ODM. Madai yake yanakaribiana na shutuma zilizoelekezwa kwa Uhuru na baadhi ya wanasiasa wa Azimio kuwa "alijitokeza sana kuunga mkono Raila" na hivyo kufanya aonekane kama "mradi" wa serikali.

Walisema hiyo, kwa kiwango fulani, iliathiri nafasi ya Raila kuingia Ikulu.

...Endelea Uk 6

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

UMOJA WA VIGOGO UTADUMU?

# Shida ya kuvuta pumzi Azimio

...Kutoka Uk 5

Hali hii ambapo wanasiasa wa Azimio wanatoa kauli kinzani za kisiasa, inatoa nafasi kwa wanasiasa wa Kenya Kwanza kuilemaza zaidi Azimio. Duru zinasema Rais Ruto anajitahidi kuchochea mgawanyiko kati ya Raila na Uhuru kwa manufaa yake ya kisiasa.

Hii ndiyo maana Seneta wa Kitui Enoch Wambua anasema kuwa masuala yote ndani ya muungano wa Azimio yatashughulikiwa.

Wambua, ambaye ni Naibu Kiongozi wa Wachache katika Seneti, anasema kuwa wanaodhani Azimio itasambaratika wanaota "ndoto ya mchana".

Anashikilia kuwa muungano huo ndio mkubwa zaidi nje na ndani ya mabunge yote mawili - Bunge la Kitaifa na Seneti.

"Kwa misingi ya nafasi ya kidemokrasia, nafasi hiyo ni kubwa zaidi ndani ya Azimio kuliko miungano mingine. Tumejitolea kuhakiki utendakazi wa serikali kwa njia inayoheshimu sheria," akasema Wambua.

Akihutubia wabunge wa Azimio katika mkahawa wa Stoni Athi, Kaunti ya Machakos juzi, Raila aliwahimiza wabunge na maseneta wa muungano huo wadumishe umoja.

Raila, Kalonzo na Karua pia waliwaonya wabunge hao dhidi ya kushawishiwa kuhamia Kenya Kwanza wakisema kitendo hicho ni "usaliti kwa raia".

Walitoa kauli hizo wakifahamu vyema kuwa Ruto anaweza kuvunja kabisa Azimio kama sehemu ya mpango wake wa kuongoza bila upinzani na kuboresha nafasi yake ya kushinda tena katika uchaguzi mkuu wa 2027. Ruto anafahamu kuwa Azimio, chini ya uongozi wa Uhuru na Raila, ni tishio kubwa kisiasa.

Wadadisi wa siasa wanasema hii ndiyo maana kiongozi huyo wa Kenya Kwanza anatamani zaidi kufaulu kutenganisha "ndugu hao wawili". Wanasema hii ndio maana, alipoapishwa kuwa Rais wa tano nchini, Ruto alimteua mtanguliza wake kuwa balozi wa amani nchini Ethiopia na eneo la Maziwa Makuu.

Kulingana na itifaki, Uhuru ataripoti moja kwa moja kwa Rais - hali ambayo itatoa nafasi kwa wawili hao kuwa na muda wa kushauriana kwa karibu.

Lakini utata umeibuka baada ya washirika wa Uhuru, hasa mwana-mikakati wake, Mutahi Ngunyi, ambaye juzi alisema Uhuru "anafurahi kustaafu". Ngunyi, ambaye ni mchanganuzi wa siasa alimshauri Raila asitumie mikakati ya zamani kuelezea kutoridhishwa na Ruto, akisema haitazaa matunda. Isitoshe, ushauri wa Ngunyi kuwa Raila anafaa kuunga mkono umoja wa kitaifa umeibua mseto wa hisia kutoka kwa wafuasi wa Azimio.

Mbunge wa Embakasi Mashariki, Babu Owino, amedai kuwa ODM "ilichezewa shere". Madai haya yalimemkwaza Kioni na wanasiasa wengine wa Mlima Kenya ambao walipoteza viti vyao kwa kumuunga mkono Raila.



Wabunge wa muungano wa Azimio la Umoja - One Kenya wakiongozwa na mwenyekiti wa ODM John Mbadi (katikati), wahutubia wanahabari jijini Nairobi mnamo Agosti 14.
PICHA | DENNIS ONSONGO

Kioni, ambaye alikuwa mbunge wa Ndaragua, anasema yeye na wanasiasa wengine waliogombea viti kupitia Jubilee na Narc Kenya, walijitolea mhanga kusimama na Raila na wakapoteza. Hesabu kutoka Mlima Keny inaonyesha Raila alipata kura nyingi kutoka eneo hilo mwaka huu kuliko miaka ya nyuma alipogombea urais.

Kwa mfano katika Kaunti ya Kiambu, alipata kura 210,393 ikilinganishwa na 69,190 mnamo 2017. Katika Kaunti za Murang'a na Nyeri, Raila alipata kura 73,539 na 51,939, mtawalia, tofauti na kura 9,122 alizopata Murang'a mnamo 2017 na 4,735 alizopata Nyeri.

Kwa jumla Azimio ilipata jumla ya kura 1,134,826 za urais kutoka eneo la Mlima Kenya, tofauti na kura 573,292 ambazo Raila alipata 2017 kwa tiketi ya ODM.

Kioni pia anasema idadi ndogo ya watu waliojitokeza kupiga kura eneo hilo ilimfaidi Raila. Hali hiyo ilichangiwa na wito wa Uhuru kwa wakazi kuwa wasimpigie kura Ruto.

Kando na Azimio, dalili zinaonyesha kuwa haja kuu ya Jubilee ni kufufua ushawishi wake katika eneo la Mlima Kenya na kuyeyusha ushawishi wa Ruto.

Shida inayokumba Jubilee si ya kipekee tangu mfumo vyama vingi uliporudi 1992, kwani imekuwa ikikumba vyama tawala. Kanu ilianza kusambaratika ilipotoka mamlakani mnamo 2002 baada ya kushindwa na muungano wa Narc chini ya Mwai Kibaki. Baadaye 2013, chama cha Party of National Unity (PNU), alichotumia Kibaki kutetea kiti chake 2007, pia kilisambaratika alipostaafu 2013. Jubilee inaonekana kufuata mkondo huo.

Vyama vikuu ndani ya Azimio vinakumbwa mvutano wa viongozi fulani kwa misingi ya mabadiliko katika ulingo wa siasa nchini.

Kwa mfano, Raila anayeongoza chama kilicho na wabunge ndani ya Azimio, anatarajiwa kumpisha kiongozi mwingine.

Kalonzo, ambaye amemuunga mkono Raila mara tatu mfululizo, anatarajia kuungwa mkono 2027 ingawa Karua anahisi ndiye "mrithi" wa Raila. Kulingana na Seneta Wambua, asasi za uongozi katika Azimio, bado zipo na majukumu yake hayajabadilika.

Huku masilahi na mandhari ya kisiasa nchini yakiendelea kubadilika kwa kasi, inasubiriwa kuonekana iwapo umoja utadumu ndani ya Azimio.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Kenya

■ NI LAZIMA SERIKALI IFANYE KAZI


# ‘BADO MAPAMBANO’, BABA AAMUA

● Na KWENDO OPANGA

Mgombea urais aliyeshindwa Raila Odinga ana hasira, amekata tamaa na ameingiwa na hofu. Amakasirika kwa sababu kwa misingi ya uchaguzi, anaamini anadhulumiwa zaidi. Anaamini alishinda chaguzi nne za urais kati ya tano alizoshiriki. Lakini hajawahi kutangazwa mshindi.

Amekata tamaa kwa sababu jinsi mambo yanavyobadilika kisisisa ndivyo yanavyozidi kubaki pale pale.

Raila amekuwa mstari wa mbele katika juhudi zote zilizoleta mafanikio yote makubwa ya kisiasa Kenya, lakini washirika wake wanasema wapinzani wake wanaoneka wameamua kufutilia mbali mafanikio hayo katika kila kipindi cha uchaguzi.



Na ameingiwa na hofu kwa sababu, kulingana na mshauri wake wa masuala ya mawasiliano Dennis Onyango, Rais William Ruto na Naibu wake Rigathi Gachagua wanawakilisha tishio kubwa kwa demokrasia nchini Kenya kuliko namna baadhi ya Wakenya wanavyoona.

“Anawaona kuwa watu wanaoongozwa na pupa ya kuvutia makundi fulani ya wanajamii upande wao kupitia amri na matamshi wanayotoa. Anahisi kuwa kuwaruhusu Ruto na Gachagua kuendeleza njama hiyo kutaleta madhara kwa taifa hili, kwa hivyo ni sharti wadhibitiwe,” anasema Onyango.

Bw Onyango alikuwa akizungumzia hatua ya Rais Ruto kuipa Huduma ya Polisi Nchini (NPS) uhuru wa kusimamia fedha na kutangaza nyongeza ya fedha kwa Idara ya Mahakama bila kuhusisha Bunge.

*Raila anavyopenda kusema, uamunifu wake kwa misingi ya demokrasia na ulinzi wa uhuru wa raia hautavunjwa na matokeo ya uchaguzi. Kwamba viongozi huja na kuondoka, lakini mapambano yataendelea*

Bw Odinga anawaona Ruto na naibu wake kuwa viongozi wanaowakilisha kurudi kwa utawala dhalimu wa Kanu chini ya uongozi wa Rais Daniel Moi Hii ni licha ya kwamba Rais Ruto amewahi kuwa mwanachama wa chama cha ODM anachoongoza Bw Odinga.

Kwa hivyo, ingawa uwezekano wa Raila kuwania urais kwa mara ya sita ni mdogo, ushawishi wake katika ulingo wa siasa utaendelea kuwepo kwa muda mrefu. Inatarajiwa kuwa ataendelea kutekeleza wajibu anaoelewa vyema wa kukosoa utendakazi wa serikali.

Baada ya kampeni kali na kupoteza katika uchaguzi wa urais kwa mara ya tano, na wengi kudhani amekwisha kisiasa, Odinga, 77, bado anaonekana mkakamavu kisiasa.

Ingawa sauti yake nyakati fulani huonekana dhaifu, bado anaonekana mwenye nguvu na ujasiri wa kuendelea kupambana.

Awali, Raila alitumia “silaha” anazofahamu vizuri za maandamano barabarani, uasi dhidi ya serikali, kususia bidhaa na huduma zinazozalishwa na watu anaoamini kuwa maadui wa demokrasia. Je, Baba (Odinga anavyofahamika) ataongoza maandamano barabarani?

Wafuasi wake wanaamini akiitisha maandamano wataendelea kumfuata. Lakini wengine wanahisi anafaa kutafuta na kuteua mwanasiasa mchanga ili amkuze na kumwezesha kuendeleza mapambano hayo.

Miongoni mwa wanasiasa hao wachanga ni wabunge Junet Mohamed (Suna Mashariki) na Babu Owino (Embakasi Mashariki). Wengine ni Seneta Enoch Wambua na Mbunge Maalumu Sabina Chege, ambao ni wanachama wa vyama vya Wiper na Jubilee, mtawalia. Vyama hivyo ni washirika wa muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya.

Raila amewataka wabunge wa Azimio wahakikishe kuwa serikali inawajibika kwa kumulika utendakazi wake kila mara.

Akihutubia wabunge wa muungano huo, aliwataka watambue wao ni sehemu ya serikali kwa sababu ni wanachama wa Bunge, asasi ambayo ni mojawapo ya nguzo za serikali.

Nje ya Bunge, Azimio inatarajia kuwa aliyekuwa Makamu wa Rais, Kalonzo Musyoka, ambaye ametangaza kuwa atawania urais 2027, atajitwika wajibu wa kukosoa serikali. Atafanya hivyo, huku akijijengea sifa na hadhi kama kiongozi wa serikali inayosubiri kuingia mamlakani.

Kwa hivyo, uwanja wa vita ambavyo Odinga ataendesha dhidi ya serikali ya Ruto ni barabarani na bungeni. Mahasidi wake watakuwa Rais, Naibu wake, Mahakama ya Upeo na Idara ya Mahakama kwa jumla na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC).

Raila amekuwa akishambulia Idara ya Mahakama na Jaji Mkuu Martha Koome, ambaye pia ni Rais wa Mahakama ya Upeo.

Amependekeza mageuzi katika Idara ya Mahakama, ambayo anasema ni mateka wa Serikali Kuu; ambayo anadai inaendeleza hongo na uhalifu. Shutuma zake zinakumbusha kuhusu lugha iliyotumiwa na Mahakama ya Upeo ilipoamua kesi ya kupinga ushindi wa Rais Ruto mnamo Septemba 5.

Kwa kilichoonekana kuwa dharau, Koome alitaja baadhi ya ushahidi uliowasilishwa na mawakili wa Odinga kuwa “hewa moto”, “ghushi”, “uvumi” na “makisio” yasiyo na mashiko yoyote. Jaji Mkuu pia aliwashutumu mawakili hao kwa kuchukulia mahakama hiyo kuwa “isiyo na umakini wowote kwa kuwasilisha ushahidi bandia”

Raila alimsuta Koome kwa kuharibu ndani ya mwaka mmoja, kazi nzuri iliyofanywa na watangulizi wake kwa miaka 10. Lakini Onyango anasema hasira za bosi wake hazitokani na kutupwa kwa kesi yake tu. “Jaji Mkuu David Maraga mnamo 2017 alielezea jinsi uchaguzi unapaswa kuendeshwa. Lakini Koome anaturudisha katika mahakama ya Willy Mutunga (2013) ambayo haikuwa na ufafanuzi kama huo.” anaeleza.

Raila ameshangaa jinsi majaji saba wa Mahakama ya Upeo walitupa malalamishi yote tisa kwa mpigo.

Alipohutubu katika mazishi Kaunti ya Meru baada ya uamuzi huo, Koome alitaja uamuzi wa pamoja wa Mahakama ya Upeo kuwa kazi ya Mungu, lakini Odinga aliutaja kuwa kazi ya shetani.

Raila ameelekeza shutuma sawa kwa mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), Wafula Chebukati. Amedai, bila kutoa ushahidi, kuwa Chebukati alihongwa na kubadili uamuzi wa Wakenya kwa kuendesha uchaguzi uliojaa dosarii.

Mashambulio haya makali dhidi ya Rais, Koome, Idara ya Mahakama na Chebukati yamewaacha wengi na maswali kuhusu iwapo Raila ameibuka upya. Haitakuwa ajabu. Raila amebadili miungano ya kisiasa na mikakati ya kupigania demokrasi, haki na mamlaka. Lakini, anavyosema mara nyingi, uaminifu wake kwa demokrasia, utetezi wa haki za raia zitabakia, na viongozi watakuja na kuondoka, lakini mapambano yataendelea.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

KUDHIBITI MAMLAKA

# RUTO ALEMAZA UPINZANI

*Muungano wa Kenya Kwanza umenyakua nyadhifa zote za uongozi katika mabunge yote mawili, hali ambayo imeuacha mrengo wa Azimio la Umoja –One Kenya pabaya. Je, ni nani atakuwa akikagua na kufuatilia utendakazi wa Serikali?*

• Na MACHARIA GAITHO

RAIS William Ruto anaendelea kusisitiza kuwa anathamini Upinzani wenye nguvu, ambao utakuwa ukiikosoa serikali yake kila inapokosea.

Hata hivyo, amechukua hatua za haraka kuhakikisha muungano wake wa Kenya Kwanza unaongoza mabunge yote - Bunge la Kitaifa na Seneti.

Ni hali ambayo huenda ikampa mamlaka na uwezo kufanya atakavyo bila upinzani ama ukosoaji wowote. Mara tu baada ya kutangazwa kwa matokeo ya urais, ilionekana kuwa kiongozi wa muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya, Bw Raila Odinga, alikuwa na idadi kubwa ya wabunge katika Bunge la

Kitaifa, na pia uwezekano mkubwa wa kuongoza Seneti. Lakini kwa kutumia mbinu alizotumia 'mwalimu' wake wa siasa, marehemu Daniel Moi katika uchaguzi mkuu wa 1992, Rais Ruto aliwashawishi wabunge na maseneta waliochaguliwa kwa baadhi ya vyama vilivyo katika Azimio wajiunge na Kenya Kwanza.

Wakati huo, Mahakama ya Upeo bado haikuwa imetoa uamuzi kuhusu kesi ya kupinga matokeo ya urais iliyokuwa imewasilishwa na

Bw Odinga. Hatua hiyo ilibadilisha kila kitu.

Mnamo Septemba 8, siku tatu baada ya ushindi wa Rais Ruto kuhalalishwa na mahakama hiyo, Bw Amason Kingi kutoka Kenya

Kwanza alichaguliwa Spika wa Seneti baada ya Bw Kalonzo Musyoka wa Azimio kujiondoa dakika za mwisho. Kabla ya uchaguzi wa Spika, Kenya Kwanza ilikuwa na wingi wa

Seneta mmoja pekee dhidi ya Azimio. Kenya Kwanza ilikuwa na maseneta 34 nayo Azimio 33.

Hata hivyo, maseneta wengi walihamia Kenya Kwanza, hali iliyomfanya Bw Musyoka ajiondoe. Iitoshe, baadhi ya maseneta wanaomuunga mkono Raila walisusia shughuli hiyo, hatua iliyomfanya Bw Kingi kushinda kwa urahisi. Bw Kingi alipata kura 46 kati ya 66. Matokeo hayo yalionyesha kuwa baadhi ya maseneta wa Azimio walimpigia kura Bw Kingi.

Katika Bunge la Kitaifa, Azimio ilikuwa ikijipiga kifua kuwa na Wabunge wengi kuliko Kenya Kwanza. Kwa mara nyingine, baadhi ya wabunge walihama muungano huo.

Katika raundi ya kwanza ya uchaguzi wa Spika wa Bunge la Kitaifa, Bw Moses Wetang'ula wa Kenya Kwanza alipata kura 215

naye Bw Kenneth Marende wa Azimio akapata kura 130.

Ikizingatiwa hakuna mgombeaji aliyekuwa amefikisha idadi ya wabunge wanaohitajika ili kutangazwa mshindi, Bw Marende alijiondoa baada ya kuhisi angeshindwa katika raundi ya pili.

Kenya Kwanza pia ilipata Manaibu Spika katika Bunge la Kitaifa na Seneti mtawalia. Mwakilishi wa Kike katika Kaunti ya Uasin Gishu, Gladys Shollei, alichaguliwa Naibu Spika wa Bunge naye Seneta Kathuri Murungi (Meru) akatwaa nafasi hiyo katika Seneti. Kibarua sasa kimegeuka uamuzi kuhusu muungano utakaotangazwa kuwa wenye idadi kubwa ya wabunge bungeni.

Kulingana na takwimu, Azimio ina idadi kubwa ya wabunge. Hata hivyo, idadi hiyo imevurugwa na wabunge wengi ambao wamejiunga na Kenya Kwanza.

Hali hiyo imezua mgogoro. Licha ya wabunge hao kuhamia Kenya Kwanza, kisheria bado wako katika Azimio, kwa sababu hawajafanya hivyo kwa kufuata sheria.

Rekodi za Msajili wa Vyama vya Kisiasa inaonyesha kuwa bado wako katika muungano wa Azimio.

Baadhi ya viongozi ambao wamejipata katika hali hiyo ni Seneta Ali Roba (Mandera), aliyehama Azimio hadi Kenya Kwanza kupitia chama chake cha United Democratic Movement (UDM).

Bw Kingi pia yuko kwenye mkanganyiko huo. Chama chake cha Pamoja African Alliance (PAA), kilijiondoa Azimio na kujiunga na Kenya Kwanza wiki chache kabla ya uchaguzi mkuu.

Ijapokuwa Msajili wa Vyama vya Kisiasa, Bi Agnes Nderitu, amesema vyama vya UDM na PAA viko katika Azimio


kisheria, hajaelezea iwapo hali hiyo inafanya muungano huo kuwa wenye idadi kubwa ya wabunge bungeni. Vyama hivyo viwili vimeenda mahakamani, vikitaka kutangazwa kuwa huru kujiunga na Kenya Kwanza, bila kufugwa na mkataba wa kisiasa katika Azimio.

Hata kabla ya Mahakama Kuu kutoa uamuzi huo, kibarua kikuu kimeachiwa Bw Wetang'ula, kuhusu uamuzi na mwelekeo atakaotoa. Bw Wetang'ula anatazamwa na karibu kila mtu kuhusu iwapo ataweka kando mwegemeo wake wa kisiasa kwa kutoa "uamuzi wa busara" kama aliotoa Kenneth Marende mnamo 2009 wakati wa Serikali ya Muungano kati ya marehemu Rais Mwai Kibaki na Raila.

Wakati wa mzozo huo, Kibaki alimteua Kalonzo (akiwa Makamu wa Rais) kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Bunge.

Lakini Raila alipinga akisema ndiye aliyefaa kupewa nafasi hiyo ikizingatiwa alikuwa Waziri Mkuu na wa pili kwa mamlaka baada ya Rais Kibaki.

...Endelea Uk 23



**Spika mpya wa Bunge la Kitaifa, Moses Wetangula, akiongoza kikao cha bunge hilo mnamo Septemba 8, 2022.** PICHA | JEFF ANGOTE | NATION

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ MWINDAJI ALIPOGEUKA MWINDWA

# MWANAMKE 'ALIYEMPIKA MAMBA'


PICHA | DAVID MUCHUI

*Kawira Mwangaza aliwashinda vigogo Kiraitu Murungi na Mithika Linturi kwa ugavana katika Kaunti ya Meru, kwa kupeleka kampeni zake kwa wananchi maskini na kutoa michango ya bidhaa kama sare za shule, madawati, blanketi na viatu*

● Na GITONGA MARETE

Gavana Kawira Mwangaza wa Meru si mwanasiasa aliyetarajiwa kuwashinda vigogo wawili wakuu wa kisiasa; matajiri na wenye uzoefu mkubwa katika siasa za Meru.

Hata hivyo, alishangaza wengi kwa kumshinda mtangulizi wake, Bw Kiraitu Murungi na aliyekuwa Seneta wa kaunti hiyo, Bw Mithika Linturi.

Alipojitosa kwenye kinyang'anyiro hicho, si wengi waliotambua uwezo wake. Alikuwa amehudumu kwa muhula mmoja tu kama Mwakilishi wa Kike katika kaunti hiyo tangu 2017. Mnamo 2013, alishindwa alipogombea ubunge eneo la Buuri.

Kilionekana kuwa kibarua kikubwa kwake kuwakabili wanasiasa hao wawili kama mgombeaa huru.

Murungi alikuwa amezindua chama chake cha Devolution Empowerment Party (DEP) na kuweka "mikakati thabiti ya kampeni" ambayo ingemwezesha "kuleta msisimko wa kisiasa katika kila sehemu nchini."

Alimtaja Mwangaza kuwa "limbukeni" kisiasa. Baada ya Waziri wa Kilimo, Peter Munya, kujiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho Februari, Murungi alisema kuwa "Mungu alikuwa ashampa kiti hicho."

Kwenye kampeni, alijifananisha na "mamba", akiwaambia washindani wake "wajihadhari naye" kwani alikuwa tayari "kuwauma" wakati wowote. Hakujua ndiye angegeuka kuwa mwathiriwa.


Linturi naye alitegemea wimbi la chama cha UDA cha Rais Willia Ruto, lililovuma katika eneo la Mlima Kenya. Linturi pia aliungwa mkono na wabunge sita kati ya tisa waliochaguliwa katika kaunti hiyo. Wabunge hao waligombea nyadhifa zao kwa tiketi ya UDA.

Wakati wa kampeni ilionekana kama ushindani mkuu ulikuwa kati ya Murungi na Linturi, kwani Mwangaza hakuweka mabango au picha zake katika maeneo ya umma.

Licha ya mbwembwe za wawili hao, Mwangaza aliwabwaga kwa kupata kura 209,148. Linturi alikuwa wa kwa kura 183,859 huku Murungi akivuta mkia kwa 110,814.

Mwangaza aliendesha kampeni zake kwa kwenda nyumba hadi nyumba. Alikita kampeni zake kwa watu wa kiwango cha chini kupitia mpango wake wa 'Operation Okolea.' Kupitia mpango huo, alikuwa akitoa michango ya vifaa kama vile sare za shule, madawati, blanketi na viatu.

Pia aliwajengea nyumba watu maskini na kutoa ufadhili wa masomo kwa watoto werevu.



Alivumisha shughuli hizo kupitia kituo chake cha televisheni cha Baite, kinachosimamiwa na mumewe, Bw Murega Baicu.

Alitoa misaada ya ng'ombe wa maziwa kwa familia maskini, huku akiahidi kuinua maisha ya watu wa mapato ya chini kama wauzaji mboga na wahudumu wa boda boda kama angeshinda.

Kupitia njia hizo, alipata umaarufu miongoni mwa watu wa kiwango cha chini, hali iliyomwezesha kushinda ugavana.

Mwangaza alidhihirisha ubabe wake wa kisiasa mnamo 2017, alipomshinda Bi Florence Kajuju kwa kiti cha Mwakilishi wa Kike. Hiyo ni licha ya kampeni kali zilizoendeshwa dhidi yake na Murungi na washirika wake katika Chama cha Jubilee.

Baada ya kuchaguliwa, alianza kutangamana na wakazi katika kila sehemu ya kaunti, hali inayoaminika kuchangia ushindi wake. Alikuwa akiendesha harakati zake kupitia Hazina ya Kitaifa ya Wawakilishi wa Kike (NGAAF) na mpango wa 'Operation Okolea.'

"Gavana alipokuwa akikutana na matajiri mjini Meru, nilijumuika na watu vijijini. Nilihakikisha pesa nilizopata kupitia hazina ya NGAAF zilitumiwa na kusambazwa vizuri," akasema.

Kwa Mwangaza, ushindi wake haukumshangaza bali ni kutimia kwa "utabiri uliokuwa umetolewa." Ni askofu wa kanisa lake la Baite Family Fellowship Church. "Nilikuwa nimemwambia Murungi hangeshindwa tu kuhifadhi kiti chake, bali angeibuka wa tatu. Pia nilimwambia ningemshinda kwa kura nyingi sana. Hayo yaliyotimia," akasema Gavana Mwangaza nyumbani kwake eneo la Makutano.

Mumewe, ambaye ni mwanamuziki wa injili, alimfaa sana kwenye kampeni. Anasema alichangia nusu ya ushindi wa mkewe. Baicu alikuwa akitunga nyimbo zenye jumbe za kisiasa ili kuchangamsha wananchi.

Mwangaza, 43, alizaliwa katika eneo la Ontulili, Kaunti Ndogo y Buuri, Kaunti ya Meru. Alisomea huko ingawa alishindwa kuendelea na masomo katika shule ya upili kwa kukosa karo. Alihamia Marsabit kuishi na shangazi yake.

"Baada ya mwaka mmoja, shangazi yangu alinipeleka Shule ya Upili ya Moyale. Miaka minne baadaye, niliibuka mwanafunzi bora zaidi katika wilaya ya Marsabit, kwa kupata alama ya C+. Baadaye nilosomea shahada ya ualimu na utoaji ushauri katika Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala," akasema Mwangaza.

Alianza biashara kkwa kuuza mboga katika soko la Kiirua. Baadaye, alifungua duka la kuuza vifaa vya ujenzi. Ni kupitia duka hilo ambapo alipata kandarasi ya kusafirisha na kusambaza simiti.

Baada ya kukosa ubunge wa Buuri 2013, alirudi kwa biashara yake. Mnamo 2015 alizindua kituo cha televisheni cha Baite.

Wakosoaji wamemlaumu Mwangaza kwa kutoshirikiana na viongozi wengine wa kisiasa, ingawa anapuuza kauli hiyo. "Kama kufanya kazi peke yangu kulinisaidia kushinda, niko tayari kuendelea kufanya hivyo. Kiraitu alishirikiana na watu waliosoma lakini akashindwa kutimiza ahadi zake," anasema Mwangaza.

Lakini kulingana na Profesa Gitile Naituli, mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Multimrdia, Mwangaza anapaswa kushirikiana na viongozi wengine katika utawala wake.

"Ameangusha vigogo. Lakini ana kibarua cha kuunganisha watu wa Meru kwa kushirikiana na viongozi wengine waliochaguliwa.

*-Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*


ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ ANACHOPASWA KUFANYA KUFUFUA UCHUMI

# UCHUMI: MUONGOZO KWA RUTO

*Kufufua uchumi wa Kenya kunahitaji mawazo mapya, ukuaji ukiwa juu ya ajenda inayofuata mkondo wa mapato na ajira*




Wafuasi wa Rais William Ruto katika Uwanja wa Kimataifa wa Michezo wa Moi, Kasarani, mnamo Septemba 13. Huku kukiwa na upungufu wa nyumba milioni mbili, karibu asilimia 61 ya wakazi mijini wanalazimika kuishi katika mitaa ya mabanda. Kenya Kwanza inaweza kuiga mpango wa SWF kutimiza manifesto yake ya nyumba za bei nafuu kwa Wakenya.

● Na MBUI WAGACHA

Kuanzia mfumo mkuu wa uchumi hadi sera za kila sekta, kufufua uchumi wa Kenya kunahitaji mawazo mapya, ukuaji ukiwa juu ya ajenda katika mkondo wa kuongeza mapato na ajira.

Mambo matatu muhimu ni pesa za umma, uwekaji akiba na shughuli za benki. La kwanza imevurugika; la pili ni hafifu kama alivyosikitika Rais William Ruto akiwa Naivasha juzi; la tatu linatumia hali mbaya ya uchumi ili kupata faida nono. Mtu anaweza kushawishika kulaumu Wakenya kwa mambo haya matatu. Lakini ni waathiriwa tu.

Fedha za Umma: Inaweza kuitwa Kamati ya Bajeti ya Rais au baraza la fedha, kwa kuweka bajeti ya kutosha na kutekeleza ajenda iliyomwezesha kushinda uchaguzi, au hata kuteua Afisi ya Bajeti na Usimamizi kama ya Amerika. Kukosekana kwa jukumu hili ambalo rais aliyeondoka aliahidi kuanzisha, kisha akaacha, kumechangia kwa kiwango kikubwa upunjaji na uporaji wa pesa za umma na kuenea kwa dosari za kifedha.

Mbali na makosa katika mambo ya kimsingi ya uchumi (kuondoa ushuru wa petroli na ada, ruzuku na ushuru wa forodha kwa kampuni za kusaga unga wa mahindi zinazofaidi wenye meli za mizigo za kutiliwa shaka katika bahari kuu kuliko wakulima wa mahindi Kenya) mikopo ilizidi.

Madeni yalipoongezeka na kukaribia Sh9 trilioni kufikia Aprili 6, 2021( karibu asilimia 65 ya mapato ya nchi), shirika la habari la Deutsche Welle lilishangaa: "Je kuna mantiki yoyote kwa IMF kupatia mikopo serikali ambazo zimedhihirisha wazi kukosa uwazi wa matumizi?"

Wakati huo, Mwelekezi wa Bajeti alidai kuwa katika mwaka wa matumizi ya pesa wa 2020 -21, Kenya ilikuwa ikikopa Sh3.37 bilioni kwa siku. Madai hayo yaliibua mengine kuwa Kenya "likuwa ikitumia pesa za watu wengine". Tunapaswa kupiga mikopo breki na kuhamisha utayarishaji wa bajeti kutoka Wizara ya Fedha hadi idara yenye uwezo katika Ofisi ya Rais.

Idara hiyo inapaswa kuwajibika kwa Rais na kutayarisha bajeti kitaaluma ikishirikiana na Bunge la Kitaifa. Tayari, Bunge la linatumia wataalamu wa Ofisi ya Bajeti ya Bunge. Idara hiyo inafaa kupatia rais ushauri huru kuhusu uchumi, kufanya utathmini huru kuhusu bajeti, na kusimamia utekelezaji wa bajeti na kufanya mabadiliko mara kwa mara. Inafaa kukuza ubunifu katika kuokoa pesa: Kuokoa pesa kumeporomoka Kenya kwa sababu ya madeni yetu. Hali hii inaweza kufafanuliwa kwa urahisi.

Kudorora kwa akaunti za matumizi na mtaji kunamaanisha nchi inatumia pesa kuliko uwezo wake. Inawekeza zaidi kuliko inavyookoa pesa. Upungufu ni lazima ujazwe kwa madeni, hatua hatari inayoshisha thamani ya shilingi ya Kenya.

**Ikiwa Kenya Kwanza haitajifunza kutoka kwa Rais Kibaki, ambaye pamoja na David Mwiraria aliyekuwa Waziri wa Fedha, walifufua uchumi na ukusanyaji wa mapato kutoka uchumi uliokuwa umedorora, na kupunguza pakubwa madeni ya serikali katika sekta ya kibinafsi, benki zitasubiri kwa hamu ili kunufaika na ajenda ya rais na Hazina ya Mahasla.**

Njia moja ya kuepuka mikopo ni kuongezea mapato, ajira na kuokoa pesa kwa kuzingatia mifumo isiyo ya madeni.

Sekta ya mali asili ya Kenya inaweza kuwa muhimu katika mkakati huu. Rasilimali zetu ni nyingi - kuanzia mafuta, titanium, niobium, magadi na madini mengine adimu sana ulimwenguni. Inahitaji mkakati unaozingatia njia mbili: Kubadilisha kandarasi na wawekezaji ili kupata faida zaidi; na kusimamia mapato

Nilipoalikwa kuzungumza jijini Washington, Amerika, nilishuhudia nguvu za nchi zingine za Afrika katika kuendeleza Hazina zao Kuu za Utajiri (SWF) kwa ukuaji wa ndani na nje ya mipaka.

Mkutano huo wa maafisa wa ngazi za juu uliokuwa na mada 'Kutia nguvu Jukumu la Hazina Kuu za Utajiri Afrika katika Mifumo ya Kifed-

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## kurunzi ya kenya

ha ya Kimataifa', ulionyesha uwezo mpya ambao serikali ya Ruto inaweza kutumia kuongeza uokoaji wa pesa na kuepuka madeni - na kuwa na pesa za maendeleo kutoka kwa masoko ya mtaji. Lakini ni lazima tupitishe na kutekeleza Mswada huo.

Hazina Kuu ya Utajiri (SWF) ni hazina ya uwekezaji inayomilikiwa na serikali au shirika linaloanzishwa kutoka vyanzo tofauti - kama vile shughuli za bidhaa na zizokuwa za bidhaa.

Katika bidhaa, nchi inapotimiza majukumu ya wawekezaji katika kandarasi kuhusu mali asili, basi itatekeleza SWF kwa faida inayolengwa kutoka kwa mapato, na kuyasimamia kwa uthabiti, vizazi vijavyo, utekelezaji wa miradi ya maendeleo, na kadhalika.

Barani Afrika, uwekezaji wa SWF katika miradi yenye faida ya maendeleo ni kigezo muhimu katika kupunguza hatari za uwekezaji katika bara hili.

Juhudi za kuanzisha na kutekeleza SWF kutumiwa kama kichocheo cha kuharakisha ushirikiano wa uwekezaji na wawezekaji wengine wa ndani na wa kutoka nje, zikiwemo SWF zingine, kwa miradi ya mipakani.


Kuvuma kwa SWF: Hazina ya Pula Fund iliyoanzishwa Botswana mwaka wa 1994 ilikuwa ya kwanza barani, zaidi ya hazina 14 zimeanzishwa na nne ziko na thamani ya zaidi ya dola 1 bilioni za Amerika chini ya Assets Under Management (AUM). AUM kwa SWF na hazina za kibinafsi za pensheni, iliongezeka kutoka dola 11 trilioni kufikia 2015 hadi dola 15 trilioni mwaka wa 2020.

SWFs zilisaidia wakati wa janga la Covid-19 ambalo, kulingana na Benki ya Dunia, lilitumbukiza watu 40 milioni katika mataifa eneo la sahara Afrika katika umasikini.


Umuhimu wa SWF kwa ahadi ya nyumba katika manifesto ya Hasla: Mfano mzuri wa jinsi ahadi kuu za Kenya Kwanza zinaweza kunufaika na SWF ni kuhusu nyumba. Ushirikiano wa habari kati ya IFC na FONSIS, SWF za Senegal, kujenga nyumba za bei nafuu ndani ya miaka kumi, ni chombo bunifu cha kufanikisha ahadi hiyo.

Ushirikiano huo unanunua nyumba kutoka kwa wajenzi na kuwapa watu wa mapato ya chini kupitia mpango wa kukodisha na kumiliki.

**SWFs barani Afrika (dola billion 1 - Mali iliyo Chini ya Usimamizi - AUM - na zaidi)**




**Mgao wa Nyumba Zilizokamilishwa Mijini**




Kenya Kwanza inapendekeza kuongeza akaunti za kununua nyumba hadi 1,000,000, bila kutoa muda wa kufanya hivyo. Inaweza kusoma utafiti wa IFC, unaoitwa Kuunda Masoko Kenya (2019). Tofauti na kukodisha na kumiliki, tafiti ambazo zilihusisha Wakenya zinaonyesha njia ya mikopo ya benki inayofungia nje makundi ya mapato ya chini kupata mikopo ya kununua nyumba na kutengewa nyumba zinazojengwa.

Katika nilichoita katika utafiti huo kuwa 'piramidi iliyoinama' ya nyumba za bei nafuu, chini ya nyumba 50,000 zinajengwa kila mwaka.

Ni asilimia mbili ya nyumba hizo zinazotengewa watu wa mapato ya chini chini ya mpango wa kununua nyumba. Uhaba wa nyumba ukiwa karibu nyumba milioni mbili, karibu asilimia 61 ya familia katika miji zinalazimika kuishi katika mazingira duni na mitaa ya mabanda. Linganisha hii na asilimia 50 Nigeria na asilimia 23 Afrika Kusini.

SWF, inayokitwa kwa kodisha na umiliki, inaweza kuwa nzuri kuliko kulenga kuongeza idadi ya watu wanaonunua nyumba kwa malipo ya polepole ambapo benki huwa zinanyakua watu wanaozitaka kwa riba za juu hata wakati ambapo mikopo wanayopewa kutoka ndani na nje kwa riba nafuu zinawawezesha kupata nyumba za bei nafuu.

Nchini Kenya, kiwango cha juu (asilimia 83) ya nyumba nafuu zinazonunuliwa na makundi ya watu wa mapato ya juu na ya kati kilikuwa cha uwekezaji, sio kufanikisha upatikanaji wa nyumba nafuu. Jambo ambalo linatuleta kwa uwezekano wa Hazina ya Hasla ukipigwa msasa na mawakala katika mfumo wa benki.

Sekta ya benki inavyoweza kuponza Hazina ya Mahsla: Kama rais mpya anataka kufanikisha ajenda ya nyumba nafuu kwa kufanya pesa kupatikana kupitia mfumo wa benki, atavunjika moyo sana. Benki Kuu ya Kenya (CBK), ikiwa msimamizi wa viwango vya riba, kutoka Novemba 17, 2019, ilionya benki dhidi ya kurudia viwango vya riba vya zaidi ya asilimia 20 ilivyokuwa kabla ya viwango vya juu kuwekwa, kunaamisha watalazimika kutetea riba za juu za mikopo. Lakini CBK siku za hivi majuzi imebadilisha nia kuhusu suala hilo.

Kinaya ni kuwa, katika kanuni mpya za ukopeshaji wa kidijitali, CBK inalenga 'ulinzi wa watumiaji bidhaa' lakini inaacha wakopeshaji wa dijitali kuendeleza riba za juu hadi zaidi ya asilimia 3,000 kwa mwaka.

Mfumo wa sasa wa kuweka riba hauna uwazi na unahamishia CBK usimamizi wa viwango: hadi kiwango cha kushughulikia sehemu ndogo za ukopeshaji - kama vile "kuhudumia wateja' kuhusu viwango vya juu vya riba ya kukopa kidijitali.

Mambo huwa mabaya kwa wateja wa benki wanaopitishiwa huduma ya wateja. Sekta yetu nyemelezi ya benki hasa hujumuisha pesa ambazo wateja huweka katika upande wa madeni. Kisha safu mbili za mali zinahakikisha ukopeshaji mdogo kwa uchumi wa ndani.

Safu ya kwanza inahusisha serikali ambayo huwa inakopa pesa nyingi na kunyima mikopo sekta ya kibinafsi. Pesa zinazobaki zinakopeshwa kampuni kubwa za kimataifa (zilizo na wamiliki warithi wa wakoloni) kuendesha biashara na kuepuka ushindani kutoka kwa biashara za Wakenya.

Kwa wanauchumi wa maendeleo, hali inaendelea kuwa hiyo. Huu ndio uwanja wa migodi ambao 'Hazina ya Hasla' itaingia ikiwa itajaribu kutumia benki kama mawakala ili kuongeza mikopo nafuu kwa biashara ndogo na za kati.

Ikiwa Kenya Kwanza haitajifunza kutoka kwa Rais Kibaki, ambaye pamoja na David Mwiraria aliyekuwa Waziri wa Fedha, walifufua uchumi na ukusanyaji wa mapato kutoka uchumi uliokuwa umedorora, na kupunguza pakubwa madeni ya serikali katika sekta ya kibinafsi, benki zitasubiri kwa hamu ili kunufaika na ajenda ya rais na Hazina ya Hasla.

*- Tafsiri na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media


# habari kwa picha



Maafisa wa polisi wakimzuilia mwanamke jijini Moscow mnamo Septemba 21, 2022, kufutia wito wa maandamano kupinga hatua ya kijeshi iliyotangazwa na Rais Vladimir Putin. Rais Putin ametangaza kutumia wanajeshi wa akiba wa Urusi akisema ahadi yake ya kutumia mbinu zote nchini Ukraine 'haikuwa mzaha' na kugusia kuwa Urusi imejiandaa kutumia silaha za kinuklia. PICHA | AFP



Maua yakiwa juu ya Gari la Serikali lililobeba jeneza la Queen Elizabeth II, likiwasili katika Ngome ya Windsor mnamo Septemba 19, 2022, kabla ya Ibada ya Wafu kwa Malkia huyo wa Uingereza. PICHA | AFP



Picha hii iliyopatikana na mpiga picha wa AFP nje ya Iran mnamo Septemba 21, 2022, inaonyesha raia wa Iran kwenye barabara za mji mkuu wa nchi hiyo, Tehran wakiandamana kuhusu Mahsa Amini, siku chache baada ya mwanamke huyo mchanga kufa akiwa mikononi mwa polisi. PICHA | AFP



Mtaalamu wa mabomu akikagua shimo lilosababishwa na mlipuko wa kombora katika kituo cha gari moshi mjini Kharkiv, Ukraine mnamo Septemba 21, 2022, huku Urusi ikiendeleza mahambulizi dhidi ya Ukraine. PICHA | AFP



Ndege wakiwa ndani ya viota vyao wakati wa mashindano ya ndege kuimba katika jimbo la Narathiwat, kusini mwa Thailand mnamo Septemba 21, 2022. Ndege wapatao 1,500 kutoka Thailand, Malaysia and Singapore walishirikishwa katika mashindano hayo. PICHA | AFP



Picha hii iliyochangwa na Erin Johnson, ambayo ilipigwa Septemba 18, 2022, inaonyesha viwango vya juu vya maji katika eneo la bandari ya Nome, mjini Nome, Alaska. Wakazi wa miji na vijiji vilivyo magharibi ya pwani ya Alaska walikuwa wakitathmini hasara kutokana na mvua kubwa ambayo haijatokea katika eneo hilo kwa miaka mingi. PICHA | AFP

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

Jukwaa La

# Vijana

## KUOKOA MAMA ARDHI

*Sandra Ruong'o ni stadi wa kupiga picha na video anayenakili, kufunza na kuhamasisha jamii kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na jinsi ya kuyazuia.*



NAFASI YA VIJANA

# KUNASA KIZAZI CHA GEN Z

**'WANUNUZI WAJUAJI':** Wauzaji bidhaa wajue kuwa kizazi hiki kinatumia sana simu za rununu na apu kupata habari. Ndio wenye mshikamano mkubwa na ushawishi mkubwa katika jamii

• NA JACKSON NGARI



KATIKA dunia ambapo kila kitu kinaonekana kubadilika, kampuni na wauzaji bidhaa wanashauriwa kufuatilia kwa kina mabadiliko ya wateja wao, njia mpya za kibiashara zinazochipuka na kupungua kwa mbinu za zamani za kutangazia bidhaa. Changamoto kuu inayojitokeza ni mabadiliko katika matumizi ya bidhaa miongoni mwa kizazi cha sasa maarufu kama 'Generation Z.'

Hata hivyo, huenda mabadiliko hayo yakawa nafasi bora kwa kampuni na wauzaji bidhaa kuboresha mapato yao. Kizazi hicho, kinachojumuisha vijana wachanga kwa umri, ni soko kubwa kwa bidhaa za kielektroniki na nguo. Kwa sasa, ndicho kinadhibiti karibu aina zote za masoko duniani.

Vijana hao ndio "wateja wapya" katika ulimwengu wa biashara. Ili kuwavutia, ni lazima wauzaji wabuni mikakati na njia zitakazotosheleza mahitaji yao, kinyume na vizazi vya awali. Moja ya nguzo kuu inayojitokeza miongoni mwao ni uwezo wa kuhimili mabadiliko.

Licha ya kuwa vijana wachanga, ni kundi linalochangia sana kwenye mapato ya nchi. Kundi hili linashirikisha vijana waliozaliwa kuanzia mwaka wa 1997. Kulingana na tafiti kadhaa ambazo zimetolewa, kundi hilo litajumuisha asilimia 27 ya wafanyakazi wote katika mashirika tofauti kufikia mwaka wa 2025.

Wamekulia katika dunia ya kidijitali, ambapo hakuna mpaka kati ya maisha yao ya kawaida na yale ya mtandaoni. Kuwepo kwa vifaa vya kidijitali vinavyowawezesha kuingia mtandaoni kwa urahisi umewaerevusha na kuwawezesha kufanya maamuzi kuhusu bidhaa na huduma watakazotumia. Wanatarajia kuingiliana na bidhaa katika majukwaa ya kidijitali bila matatizo yoyote. Wanataka kutoa maoni yao katika njia tofauti. Wanapotoa majibu yao, kuna uwezekano kuwa wengi hutoa majibu mazuri, badala ya kulalamika

Hata hivyo, wauzaji bidhaa wengi wamekosa kubuni mikakati ya kutangamana nao ili kufahamu mahitaji yao. Katika hali hiyo, wanatarajia wauzaji bidhaa kushughulikia kwa kina mahitaji yao. Vile vile, wanataka bidhaa hizo kuwa za kweli, zinazoweza kuaminika na zinazolingana na uhalisia wa maisha yao.

Kutokana na hayo, wauzaji bidhaa wana nafasi nzuri ya kubuni mwingiliano mwafaka na kizazi hiki unaoweza kukuza na kuongeza imani yao kwa bidhaa wanazozouza. Kuaminika kwa bidhaa hizo ndiko suala muhimu zaidi. Mbali na hayo, kizazi hiki kinapendelea bidhaa zinazovutia, rahisi kutambulika na za kipekee.

Wauzaji bidhaa wengi wanasema wameanza kuhisi uzito na ushawishi wa kizazi hiki, hasa kwenye matumizi ya bidhaa. Wengi wanazitumia kulingana na wanavyoziamini.

Zaidi ya hayo, wameanza kuwa na usemi mkubwa kuhusu bidhaa wanazotaka, ambazo si lazima zilingane na umri wao. Wengi wanalenga kuongeza utajiri wao binafsi. Wana mawazo kuhusu kile wanachotaka, jinsi watakavyokipata na vile kitawafikia.

Wanataka nafasi ya kujieleza kwa muuzaji. Wanataka pia kushirikishwa katika taratibu za kutengeneza bidhaa na huduma wanazotamani. Wauzaji bidhaa wasio tayari kukielewa kizazi hiki wamo hatarini ya kupoteza mauzo na faida. Uhalisia mchungu ni kuwa: Wasioridhika na bidhaa au huduma fulani wataelekea kwingine.

Ili kuwateka na kuwaridhisha v, wauzaji bidhaa wanafaa kutafuta njia za kuhakikisha mteja amefurahishwa na ubora wa bidhaa ama huduma husika. Wanafaa kubuni mikakati inayozingatia kutimiza mahitaji ya kizazi hicho kupitia mitandao na nje ya mitandao.

Huenda vijana hao wana ushawishi mdogo kwa sasa. Lakini wameanza kushawishi familia na marafiki zao. watajenga imani katika bidhaa zako ikiwa utajumuika nao kwa njia na mbinu wanazotaka. Kwa kizazi hiki, ukweli ndiyo muhimu. Hakikisha kwamba umewaeleza kila kitu kwa uwazi kuhusu bidhaa zako.

Mwisho, wauzaji bidhaa wanafaa kufahamu kuwa kizazi hiki kinatumia sana simu za mkononi na apu za simu kununua bidhaa. Sababu kuu ni kuwa njia hizo zinawapa nafasi kuwasiliana kwa urahisi na kufanya maamuzi mazuri kuhusu aina ya bidhaa wanazotaka.

*Na: Jackson Ngari, Mwanafunzi wa Mawasiliano na Uanahabari, Chuo Kikuu cha Rongo, Migori, Kenya.*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

## WANAVYOSEMA



**Israel Lugadiru**

Ingawa hali si nzuri sana nchini, hatuko katika shimo la kina. Kiini cha matatizo yetu si mikopo mikubwa tu, bali pia kushuka kwa thamani ya shilingi ikilinganishwa na dola ya Amerika, ambayo ndiyo sarafu kuu ya biashara. Kuondolewa kwa ruzuku za mafuta kutaokoa Kenya.

*— Kiongozi wa Wanafunzi, Chuo Kikuu cha Nairobi*



**Esther Kurraru**

Tunahitaji kupanga jinsi tutaishi kwa kutegemea mapato tunayokusanya. Ukopaji mkubwa ndio umetuletea matatizo tuliyo nayo. Serikali ya Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta ilikopa sana, mtindo unaoonekana kuigwa na Wakenya wengi. Rais William Ruto anapaswa kubuni nafasi za kazi.

*— Muuguzi*



**Derrick Barnett**

Tuko katika hali mbaya sana kwani ni vigumu sana serikali kuendelea kudumisha ruzuku. Serikali inafaa kulinda ushuru wetu.

Inapaswa kukabili ufisadi ili kuimarisha utoaji huduma. Wakenya tayari wanalemewa na zigo kubwa la ushuru. Hivyo, ni vizuri serikali kuboresha utoaji huduma kwetu.

*-Muuzaji kidijitali*



**Amos Salaton**

Nchi yetu ina rasilimali nyingi sana. Tunaweza kusuluhisha changamoto zinazotuandama kwa kutumia vizuri rasilimali zilizopo, kupunguza matumizi, kubuni mfumo mahsusi wa kukabili ufisadi na kuacha ukopaji.

*-Mhudumu wa afya*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

MTAZAMO WANGU

# MOMBASA RAHA TENA

**MIZIGO:** Hatua ya kuhamisha shughuli za kontena kutoka bandari hiyo ilikuwa kitendo kikubwa zaidi cha kuvunja uchumi katika kisiwa hicho tangu Wareno walipokichoma hadi majivu miaka 500 iliyopita



• NA WAGA ODONGO




Eneo la pili la kushughulikia kontena katika bandari ya Mombasa mnamo Juni 30.
WACHIRA MWANGI | NATION

Nilipokuwa nikikua, nilisomea shule ya Tudor, Mombasa, eneo ambalo limepewa jina la nyumba ya kifalme ya Muingereza iliyobomoka zamani na ambao ungekuwa umebadilishwa jina kitambo.

Karibu na shule yetu, ukipita mtaa wa mabanda wa Moroto, tulikuwa tukienda baharini moja kwa moja. Tulipenda kwenda hapo baada ya masomo kutupa mawe ndani ya bahari kuona aliyeweza kutupa mbali zaidi.

Mkoko mdogo uliokuwa hapo ulikuwa umekauka na maji yenyewe hayangeweza kuogelewa. Yalikuwa na povu juu lililotukumbusha kiwanda cha kusafisha mafuta cha Changamwe kilichokuwa karibu.

Kiwanda hicho kiliacha kutoa moshi mchafu na kupumua moto na majengo yake yote sasa yanatumiwa kuhifadhia bidhaa lakini kina kumbukumbu itakayodumu kwa miaka mingi.

Mikoko ambayo ingekuwa eneo la kuzalia samaki sasa imekufa pamoja na uvuvi ambao ulikuwa ukifanywa karibu na kisiwa hicho. Samaki wengi wanaoliwa nchini, hasa aina ya Mackerel, ambao tunawaita 'Una', sasa wanatoka mataifa ya nje.

Ukienda katika masoko mkubwa ya samaki eneo la Old Town, utaona vipande vikubwa vya barafu vimefunika samaki warefu kuliko mtu. Samaki wanaolisha kisiwa hicho wanavuliwa hasa na mashua za kimataifa ambazo wahudumu wake ni mabaharia kutoka Ufilipino na Cameroon. Wavuvi wa humu nchini hushughulika tu na pweza na kaa - huku hao wa kigeni wakivua aina wengine wa samaki.

Huenda samaki wameisha katika bahari karibu na pwani lakini tunafaa kuelewa kuwa bandari, na meli zake za mafuta na kiwanda cha kuyasafisha kilicho karibu, imefanya mambo kuwa mabaya kwa wavuvi wachache waliobaki Mombasa, Kilifi na Kwale na imeathiri pakubwa chakula kinacholiwa pwani.

Usumbufu mwingi wa bandari hiyo haujitokezi unapoketi katika meza ya mankuli. Unakupata ukielekea nyumbani. Kila mwezi, au mara 13 kwa mwaka, meli kubwa ya mizigo ya Super Panamax hufika kubeba mizigo ya madini ya ilmenite, rutile na zircon.

Super Panamax ina urefu wa karibu kilomita moja na ina orofa kadhaa na ni lazima iendeshwe pole pole katika kivuko cha Likoni.

Wakazi wa Mombasa huvumilia usumbufu wa meli za nchi tano ambazo huvuruga usafiri wao kila wakati. Meli hizi, baadhi yake zikiwa za kivita za Amerika na Muungano wa Ulaya, zina haki ya kupita kwanza na wakazi huwa wanatazama huku feri yao ikikawia au kupita kando kuruhusu wamiliki halisi wa kivuko hicho kunufaika na matumizi yake.

Sababu ya feri kutozingatia ratiba iliyowekwa ni kuwa kivuko hicho wakati mwingine hutumiwa na meli ambazo urefu wake ni sawa na viwanja vidogo vya ndege na zina haki ya kupita kwanza.

Kuwa na bandari katika fuo kunamaanisha utapokea mashua zinazojaa shehena za mihandarati.

Kwa sasa, Mombasa ni kituo muhimu ambacho dawa ya heroin kutoka Mashariki inaingizwa nchini. Shida ya matumizi ya dawa za kulevya inashuhudiwa pwani.

Mombasa ilikuwa na kliniki ya kushughulikia waathiriwa wa mihandarati kabla ya nyingine kufunguliwa Nairobi. Matumizi ya heroin yalianzia pwani na kusambaa hadi ndani ya nchi. Mpango wa kuwapa waathiriwa sindano katika kiliniki moja ya kurekebisha waathiriwa Kisauni ulifaulu hadi nchi zingine ulimwenguni zikalazimika kuuiga.

Utashangaa ni kwa nini nchi inayokumbatia dini inaweza kuwapa watumiaji wa mihandarati sindano na maagizo ya kuzitumia. Naam, utafiti ulifichua kuwa kiwango cha HIV katika watumiaji wa dawa za kulevya ni karibu mara tano ya kiwango cha kitaifa.

Pamoja na habari hizi za mahangaiko ya kiuchumi ambayo yaliandamana na kuhamishwa kwa shughuli za kontena hadi bara, shida hizo bado ziko. Kuhamisha shughuli za kontena kutoka bandari hiyo kilikuwa kitendo kikubwa zaidi cha kuvunja uchumi katika kisiwa hicho tangu Wareno walipokichoma hadi majivu miaka 500 iliyopita.

Mombasa na vitongoji vyake inabeba mzigo na makovu ya kuwa na bandari hiyo na manufaa ya kushughulikia mizigo lazima yarudishwe kwa wakazi.

Kontena huchukua wiki kadhaa kwenye bahari zikisafirishwa kilomita 30 kwa saa. Kwa nini zisafirishwe ghafla kwa kasi ya juu kwa treni?

Sio tu wenye hoteli na wafanyakazi wa kampuni za kuondoa na kusafirisha mizigo wanaosumbuliwa na agizo hilo, ni kila kitu ambacho kiliibuka kusaidia bandari hiyo. Uamuzi kuwa Huduma za Kontena ziwe kilomita 10 kutoka bandarini umefanya gharama ya maisha karibu na eneo hilo la Mombasa kupanda.

Mfumo wa kuondoa makontenea umekumbwa na kashfa tele - biashara ya ufisadi. Lakini suluhisho si kusafirisha makontena yote hadi Nairobi na Naivasha. Je, shughuli za uondoaji zinaweza kuhalalisha kuhamishwa kwa sekta nzima iliyochukua karne kadhaa kujenga?

Bandari inaletea serikali pesa nyingi kuliko Nairobi. Kile ambacho serikali inaweza kufanya ni kuhakikisha shughuli zake zinabaki Mombasa.

Hatuwezi kufanya manufaa ya bandari kuwa ya kijamii kwa kuita mali ya taifa, ilhali usumbufu, kupotea kwa nafasi za ajira na janga la uchafuzi wa mazingira zinaathiri watu wa Mombasa.

Rais Ruto amerudisha Shughuli za Bandari Mombasa zinakopaswa kuwa, hazikufaa kuondolewa kamwe.

*Bw Odongo ni mhandisi wa programu za kompyuta.*

*- Tafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

KAMERA MKONONI, KUOKOA DUNIA YETU

# KUZUIA MABADILIKO YA TABIA NCHI

**INAWEZEKANA:** Sandra Ruong'o anaamini wapiga picha, wachukua video na wasanii wengine wana wajibu mkubwa wa kuhamasisha jamii kuhusu madhara ya tabia nchi kijamii, kiuchumi na kisiasa



Bi Sandra Ruong'o, mpiga picha na video ambaye anashughulikia masuala ya mabadiliko ya tabia nchi na jinsi ya kuyazuia, akihutubia wageni katika hafla ya 'Mashujaa wa Kike wa Tabia Nchi eneo la Westlands, Nairobi, mnamo Machi 25.

• NA HILARY KIMUYU

Sandra Ruong'o ni mwanamke anayeridhika na hali yake na vitu vyote vinavyomzingira. Lakini pia ni mwanamke mwenye wajibu wa kufanya mabadiliko ya tabia nchi kuwa ajenda ya kila mtu.

Akiwa na umri wa miaka 32, Sandra amehudumu kama mtaalamu wa mawasiliano, mpiga picha na mtengeneza filamu kwa kutumia picha za kufurahisha na simulizi zinazoleta mabadiliko kwa watu.

"Kuleta mabadiliko ndani ya watu ndiko kunahitajika ili kuokoa ulimwengu wetu. Hatufai kusimama tulipo au kurudi nyuma," akasema.

Jinsi mabadiliko ya hali ya hewa yanavyozidi kuwa jambo la dharura, ndivyo nafasi ya upigaji picha za kuhamasisha inajitokeza.

Hata hivyo, kwa watu ambao hawajaathiriwa moja kwa moja na madhara ya ongezeko la joto ulimwenguni, suala hilo halitaeleweka vizuri.

Kulingana na Sandra, picha kuhusu hali ya hewa husiadia kuthibitisha uhalisia wa kile ambacho awali kilidhaniwa tu.

Mwanahabari huyo mpiga picha anayeishi Nairobi, hunakili, kufunza na kuhamasisha kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na namna ya kuidhiti madhara yake.

"Ipo haja kwa wapiga picha barani Afrika kuonyesha athari za mabadiliko ya tabia nchi na juhudi zinazofanywa na watu, serikali na jamii mbalimbali kuzizuia. Nalenga kuangazia madhara ya mabadiliko ya tabia nchi barani Afrika nan je kijamii, kiuchumi na kisiasa."

Akiwa na tajriba ya miaka mingi katika sanaa ya upigaji picha katika mataifa mbalimbali Afrika, kazi za Sandra huangazia mabadiliko ya tabia nchi, siasa, jinsia na maendeleo.

Mwaka huu, aliandaa maonyesho yake ya kwanza ya picha kwa jina, "Climate Heroines" (Mashujaa wa Kike wa Tabia Nchi) kuwaenzi na kuangazia wajibu wa wanawake katika juhudi za kupambana na madhara ya tabia nchi.

Maonyesho hayo yalijumuisha wanawake tisa na kundi la wanawake. Sadra alitaja maonyesho hayo kuwa kilele cha taaluma yake.

Ingawa shughuli hiyo ilihitaji pesa nyingi, alipata misaada ya kutosha ambayo ilimwezesha kuendelea kuelezea matukio mbalimbali kwa picha.

"Natarajia kuelezea habari nyingi kuhusu wanawake wanaohusika katika juhudi za kudhibiti wa tabia nchi kwa sababu kuna wengi kule nje ambao wanafanya kazi nzuri. Kwa sababu Novemba ni "mwezi wa wanaume" nitawaenzi wanaume kwa kuandaa maonyesho kwa jina "Climate Heroes" (Mashujaa wa Tabia Nchi".

**Akiwa na tajriba ya miaka mingi katika taaluma ya upigaji picha katika mataifa tofauti ya Afrika, kazi ya Sandra huangazia mabadiliko ya tabia nchi, siasa, jinsia na maendeleo. Mwaka huu aliandaa maonyesho yake ya picha kwa jina "Climate Heroes" (Mashujaa wa Tabia Nchini) kuenzi na kuangazia mchango wa wanawake katika kuendeleza na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.**

Picha hizo, Sandra anasema, zinapitisha ujumbe muhimu lakini pia zinavutia hisia za wanaozitazama.

Vile vile, wapiga picha wa masuala ya mabadiliko ya tabia nchi wanachangia data muhimu kwa wanasayansi. Hii ni kwa sababu picha zao zinasaidia katika kufuatilia na kupima madhara ya sasa na kukisia madhara ya miaka ijayo.

"Athari za mabadiliko ya tabia nchi hujitokeza polepole kiasi kwamba haziwezi kuonekana kwa macho. Hali ya kujirudia imewafanya watu kupuuza habari muhimu kuhusu jinsi mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri watu na sehemu mbalimbali kote ulimwenguni," anasema Sandra.

"Kunasa hata sehemu ndogo ya yale watu wanapitia kunatosha kuibua mjadala dunia nzima nilivyotarajia. Lakini tunahitaji msukumo na kujitolea kwa pamoja ili tuweze kuokoa ulimwengu wetu." anaongeza.

Huku Kongamano la 27 la Umoja wa Mataifa Kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchini likikaribia (Novemba 6 hadi Novemba 18) mijadala kuhusu suala hilo imeshika kasi katika mitandao ya kijamii.

Hii ni kutokana na takwimu ya kuhofisha kuhusu kiwango cha athari zinazowakabi-

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



Claire Nasike Akello ni mtaalamu wa mifumo ya chakula katika shirika la Greenpeace Africa. Huongoza kampeni kuhusu chakula, kufunza jamii kuhusu kilimo na mbegu zinazofaa kutumiwa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Kwa watu ambao hawajaathiriwa moja kwa moja na madhara ya ongezeko la joto ulimwenguni, suala hilo halitaeleweka vizuri na watafikiria ni dhana tu.

li wanadamu. "Wengi wetu tunafahamu kauli kuwa "picha moja ni bora kuliko maneno elfu moja". Kauli hii imeafiki wakati huu tunapoangazia madhara ya mabadiliko ya tabia nchi," anasisitiza Sandra.

"Kama picha moja inamfanya mtu kuacha anachofanya, kufikiri na kuchukua hatua, basi picha hiyo ni bora kuliko maneno elfu moja, kwa maoni yangu."

Sandra amehitimu Shahada ya Digrii katika Mawasiliano na Uanahabari kutoka Chuo Kikuu cha Maseno.

Alianza kazi yake mnamo 2014 kama mtaalamu wa kunasa video katika Mpango wa Pamoja Together, kwa ushirikino na Chuo Kikuu cha Boston, Chuo Kikuu cha Great Lakes na Chuo Kikuu cha Sayansi na Ufundi cha Jaramogi Oginga Odinga.

Mpango huo ulidhaminiwa na Wakfu wa Bill and Melinda Gates kwa ajili ya kudhihirisha manufaa ya misaada ya wafadhili kwa jamii zinazoishi maeneo ya mashambani.

Amefanya kazi na mashiriki la serikali na yasiyo ya serikali barani Afrika. Hamu yake kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabia nchi iliendela kuongezeka na ikamwezesha kupata cheti cha kitaaluma katika Biashara na Uendelezi wa Mipango kutoka Chuo Kikuu cha European Business University.

Sandra aligeukia mtandao wa YouTube na Shule ya Upigaji picha kidijitali (Digitali Photography School-DPS) kunoa talanta yake katika taaluma ya upigaji picha na unasaji video.

Aliibuka wa pili katika Mashindano ya Upigaji Picha Wanyama pori Afrika Mashariki, mnamo 2016. Mwaka uliofuata, aliajiriwa kuwa mpiga picha rasmi katika kampeni za urais za aliyekuwa Waziri Mku Raila Odinga.

Mwaka huu pia alifanya kazi na Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa jijini Geneva kuhusu Siku ya Kimataifa ya Wanawake.

Sandra anasema huwa hatumii picha zake kuendeleza maandamano au kufanya uasi. Badala yake huzitumia kuunda vitabu, kuandaa maonyesho na hafla mbalimbali za kuvutia jamii na hivyo kuihamasisha.

## Athari za mabadiliko ya tabia nchi hujitokeza pole pole baada ya muda kiasi kwamba ni vigumu kuyaona mara moja kwa kutumia macho yetu.

Sandra Ruong'o

"Tuna ulimwengu mzuri na maridadi na uliojaa mambo mbalimbali. Kwa sababu hiyo, tunafaa kuchukua hatua iwapo tunataka kizazi kijacho kifurahia kila tulicho nacho leo. Nalenga kuwapa motisha wengine ili wawe na mtazamo sawa na wangu kuhusu ulimwengu; waone ulimwengu kuwa mseto wa mimea na wanyama wanaopaswa kuishi maisha yao bila kuvugwa au kuingiliwa na shughuli za binadamu.

Sandra anashauri kuwa wakati kama huu hatuwezi kuketi na kuzungumzia ulimwengu unaokumbwa na changamoto mbalimbali.

"Sura ijayo ya maisha ulimwenguni itajengwa na hatua tunazochukua sasa. Ninapofikia umri wa miaka 33 Oktoba mwaka huu, nitapanda miti 33.

Nataka kila mtu mwenye umri mdogo hapa nchini apande miti na kuhamasisha wengine kuhusu umuhimu wa shughuli hiyo", anasema.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*



Sumaiya Harunany (kushoto) na Fatma Abdulrehaman Alimohamed kutoka Mombasa. Sumaiya ndiye mwanzilishi wa Shirika la Blue Earth. Fatma ni mwalimu, mwanamazingira na mwanzilishi - mwenza wa Shirika la Blue Earth. Huku Kongamano la Umoja wa Mataifa Kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi likikaribia (Novemba 6-18), mjadala kuhusu mabadiliko ya tabia nchi umeshika kasi kwenye mitandao ya kijamii. PICHA ZOTE | HISANI

Nation Media Group "ePaper Copy"

KUSHINDA MABAYA YALIYOPITA

# SI UREMBO TU, PIA NIA

• NA AMINA WAKO

**MWANAMKE POLISI:** Emma Brenda Wanjiru, hutumia mitandao ya kijamii kuzungumzia kuhusu mama mzazi asiye na mume, mimba za matineja na dhuluma za jinsia, akitumia tajiriba yake kuwatia moyo wengine



Konstebo Emma Brenda Wanjiru ni mmoja wa maafisa wa polisi wenye sare za kazi wanaofahamika sana nchini, kutokana na urembo wake mitindo yake maridadi ya mavazi.

Picha zake akivalia sare za polisi zilipotokea kwa mara ya kwanza mtandaoni mwaka wa 2016, wengi walishangaa ni kwa nini alikuwa akiharibu urembo wake katika taaluma inayohusishwa na ugumu na ukatili.

Lakini kuna zaidi kwa Emma kuliko kung'ara kwake na viatu vyake venye visingino virefu. Anatumia mitandao ya kijamii kuzungumzia kuhusu hali ya kuwa mama mzazi bila mume, mimba za matineja na dhuluma za kijinsia akitumia tajiriba yake ili kuwatia moyo wengine.

"Huu ndio mtazamo wangu. Mungu alinipa kiumbe. Kwa nini niaibike kwa sababu yake? Niliingia katika uhusiano mbaya na nikajifunza kutokana nao. Hufai kujihurumia ukijipata katika hali kama hiyo. Kubali hali hiyo na uendelee na maisha yako.

Nchini Kenya, karibu wasichana watano wenye umri wa kati ya miaka 15 na 19 tayari wamepata mtoto au wako na mimba, kulingana na utafiti uliofanywa mwaka wa 2014.

Mwanamke huyo mwenye umri wa miaka 33 alizaliwa na kulelewa Nyahururu akiwa kifungua mimba katika familia ya watoto wawili, Mama yao aliwalea peke yake baada ya baba ya afisa huyo wa polisi kuwaacha, Emma akiwa na umri wa miaka minne.

Mama yake, ambaye pia alikuwa katika huduma ya polisi alikuwa mkali sana lakini pia mpole. "Maadili aliyonifunza wakati huo yalinifanya kuwa mtu niliye nilivyo leo. Kama haingekuwa malezi yake, ningekuwa mtu dhaifu."

Akisoma katika Shule ya Upili ya Wasichana ya Ngiriambu, Kaunti ya Kirinyaga, Emma alikuwa akimtembelea mjomba wake eneo la Kiserian, Kaunti ya Kajiado shule zikifungwa.

Akiwa kwa mjomba wake mnamo 2008, punde tu baada ya kumaliza shule ya upili, alikutana na kupendana na kijana kutoka Ongata Rongai. Kwa msichana mbichi, safari yake ya siku za usoni ilikuwa imeanza na alijiona kuwa na maisha mazuri ya raha akiwa na urembo wake. Alipata mimba na akalazimika kuwaficha shangazi na mama yake kwa kutorokea kwa mpenzi wake. Waliishi katika chumba kimoja Rongai na mwanzoni, maisha yalikuwa mazuri. Lakini hadithi ya maisha matamu ya mapenzi haikudumu kwa muda mrefu.

"Uhusiano wetu ulibadilika sumu kwa kuwa baba ya mtoto wangu alianza kunidhulumu kwa kunipiga, kihisia na kisaikolojia," anakumbuka.

Huo ndio ulikuwa wakati mbaya zaidi katika maisha ya Emma. "Angeniambia sikuwa na maana, kuwa singeolewa kama ningemuacha, kuwa singefaulu kwa lolote na kuwa hata ningemuacha, ningerudi kwake tu. Aliniweza na nikaendelea kuishi naye licha ya kunichapa. Alikuwa na hakika singerudi kwetu kwa sababu nilimpenda sana. Nilimwamini kwa sababu alikuwa amenizidi umri. Nilijiuliza ningeenda wapi, tineja ambaye hakuwa na stakabadhi zozote, bila kazi, bila chochote. Kwa hivyo nilikaa kwake tu."

Emma alizama katika huzuni na wakati fulani akafikiria kujiua. Binti yake, Lanisha, alipokuwa na umri wa wiki nane, alipata nguvu za kuacha ndoa kwa hofu ya kuuawa akarudi kwa mama yake Nyahururu. Alitumia mwaka mzima kusahau yaliyopita na kutafuta njia ya kusonga mbele na maisha yake. Aliamua kurudi shule na akahamia Nairobi akiwa na binti yake, wakaanza maisha ypya mtaa wa Jericho, Mashariki ya Nairobi, ambako mama yake alimpangishia chumba kimoja.

Alikuwa akipeleka Lanisha katika kituo cha ulezi asubuhi na kuhudhuria masomo ya kazi na maendeleo ya jamii, na kumchukua jioni. Baada ya miezi kadhaa alipata kazi kama muuzaji katika duka.

"Nilikuwa na bidii sana, lakini nikahisi kulikuwa na kitu ambacho hakikuwa sawa na kazi hiyo. Baada ya kutafakari, niling'amua kwamba ndoto yangu ilikuwa kuwa polisi."

Nation Media Group "ePaper Copy"



Emma Brenda Wanjiru wakati wa sherehe ya kuhitimu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mnamo Oktoba 2012, Emma aliacha kazi akarudi Nyahururu kujaribu bahati yake katika usajili wa makurutu wa polisi Novemba.

"Kwa mwezi mmoja, nilifanya mazoezi kwa bidii kwa sababu nilijua kilichohitajika. Nilikuwa nikiamka mapema asubuhi na kukimbia," anakumbuka.

Aliibuka wa tano, lakini Huduma ya Taifa ya Polisi ilihitaji wanawake wanne pekee. Emma alikuwa ameomba Mungu atimize ndoto yake ya kuwa afisa wa polisi na alishangaa ni kwa nini Mungu hakujibu maombi yake. Lakini hakufaa kulalamika kwa sababu aliitwa tena jukwaani baada ya mmoja wa wanawake hao wanne kupatikana na mimba.

Na kwa hivyo, mnamo Januari 2013, Emma alijiunga na Chuo cha Mafunzo ya Polisi cha Kiganjo, Nyeri, ambako alifunzwa kwa miezi 18 na kuhitimu 2014.

"Miezi hiyo 18 ilikuwa migumu sana kwa sababu ilikuwa mara yangu ya kwanza kuishi mbali na binti yangu. Lakini nilikuwa na furaha kwa sababu ndoto yangu ilitimia. Nilihisi kuwa afisa wa polisi ulikuwa wito kwangu, na kungenifikisha katika hatua ya pili. Hatimaye nilihitimu na kila mtu alifurahia," aliongeza.

Kama kazi zingine, kazi ya polisi ina changamoto zake. Mnamo 2019, alikuwa na msongo wa mawazo na alitaka kuacha kazi, lakini mmoja wa wakubwa wake akamuomba afikirie tena uamuzi wake.

"Unafikiria kuhusu nafsi yako, lakini kumbuka, sio kuhusu wewe tena. Unakumbuka watu wote wanaokutegemea? Ukikata tamaa na kuacha kazi itakuwaje kwao?" mkubwa wake akamuuliza. Ushauri huo ulimfanya agundue kuwa alikuwa na jukumu kwa wengine zaidi ya yeye binafsi, hasa mwanawe.

"Ndiye ufanisi wangu mkubwa na ninatamsaidia kuwa bora zaidi kwa sababu ana talanta nyingi; anaweza kuimba, kucheza densi na kuwa mwanamitindo."


Emma pia anamshukuru mama yake kwa kuwa nguzo yake. Anawazia kupiga hatua zaidi katika kipaji chake cha mitindo. "Nimekuwa nikifikiria kuanzisha kampuni ya mavazi, lakini hiyo ni hadithi ya siku nyingine."

Licha ya sifa na umaarufu wote huo, Emma aliyehitimu kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, anasumbuliwa na maisha yake ya zamani. Mawazo ya kupata mimba akiwa tineja, kuachwa na baba ya mtoto wake na ndoa ya mateso kumeathiri uhusiano wake na wanaonuia kumchumbia.

"Nimekuwa mwangalifu zaidi, jambo ambalo wakati mwingine si kitu kizuri. Maisha yangu ya awali yamenifanya nikawakatae watu wazuri wanaotaka uhusiano wa dhati. Singetaka kurudi huko, ni mahali penye giza."

Kwa sasa, Emma anatumai kuwa masaibu yake yataendelea kuwapa matumaini wengine wanaojipata katika hali sawa na yake.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*




Nation Media Group "ePaper Copy"

taharīri




■ Uhuru katika matumizi ya fedha unafaa kumkumbusha Inspekta Jenerali wa Polisi kwamba hawafai kuvunja sheria ili waonekane kuitekeleza.

# Polisi wajue raia si maadui



KWENDO
**OPANGA**

Katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu uliopita, mgombea urais wa United Democratic Alliance (UDA) William Ruto na mgombea mwenza Rigathi Gachagua walionekana kuwa na hamu ya kuimarisha masilahi ya polisi.

Ajabu ni kuwa UDA na pia mrengo wa Azimio la Umoja, hawakutangaza hatua za kuzuia uhalifu na mambo yanayouchangia.

Hakuna mrengo ulioshutumu mienendo ya maafisa wa polisi ya kushiriki uhalifu au tabia yao za kudhulumu raia bila sababu.

Lakini kwa haraka, Rais Ruto alitumia mamlaka yake kuipa Huduma ya Kitaifa ya Polisi (NPS) uhuru wa kusimamia matumizi ya pesa yaliyotengewa idara hiyo.

Uhuru huu unampa Inspekta Jenerali wa Polisi mamlaka ya kuandaa, kutetea na kutekeleza bajeti ya NPS. Amepandishwa hadhi na kuwa afisa mwenye usemi katika masuala ya matumizi ya pesa.

Hapo awali, wajibu huu ulitekelezwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Usalama wa Ndani, inayosimamia NPS. Mkuu wa polisi hajawahi kupewa mamlaka kama haya katika historia ya Kenya.

Sasa makao makuu ya polisi, jumba la Vigilance, yana mamlaka ya kuamua kiwango cha pesa ambazo idara hiyo inahitaji, mahala, lini na sababu ya kutumia pesa hizo.

Swali ni je, NPS uhuru kwa matumizi ya pesa itakuwa katika nafasi ya kuwalinda Wakenya dhidi ya wahalifu? Je, polisi watakuwa wepesi kukamata wahalifu na kuwapeleka kortini? Muhimu zaidi, polisi wanataimarisha uhusiano wao na umma na hivyo kuwahudumia vizuri?

Zingatia hili. Mnamo 2020, serikali ilianzisha kafyu nyakati za usiku kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa Covid-19. Hata kabla ya ugonjwa huo kuua Mkenya yeyote, maafisa wa polisi walikuwa wameua watu wengi kwa kisingizio cha kutekeleza amri hiyo ya kafyu.

Vitendo hivyo viliibua malalamishi mengi kutoka kwa Wakenya wa matabaka mengi, likiwemo Baraza la Kitaifa la Makanisa Kenya (NCCK). Kwenye barua ya malalamishi memoranda kwa aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta, baraza hilo lilisema hivi:

"Ilivyodhihirika siku ya mwanzo baada ya mlipuko wa janga la Covid-19 nchini, inaonekana maafisa wa polisi wamedharau haki za Wakenya kwa kutumia nguvu kupita kiasi katika kutekeleza sheria ya kafyu. Wakenya wengi wamepoteza maisha yao, na wengine kulemazwa, mikononi mwa maafisa wa polisi bila sababu maalumu."

NCCK ilisema ukatili huo wa polisi ulichangiwa na hali ya kutoshughulikiwa kwa mtazamo wa polisi kwa raia na hali ya uadui baina ya polisi na umma. Polisi wanachukulia raia kuwa watu wasio na ungwana na ambao haja yao kuu ni kuvunja sheria. Kwa upande mwingine, raia wanaona polisi kuwa makatili ambao wajibu wao mkuu ni kuwadhulumu na kuwapunja pesa.

Mtazamo wa polisi ni kwamba umma ni adui. Kimsingi, maafisa wanafaa kutoa huduma lakini wanafanya kazi kwa kutumia nguvu kupita kiasi. Maafisa wa polisi hulinda masilahi ya serikali na maafisa wenye ushawishi mkubwa huku wakihujumu na kudharau masilahi na uhuru wa raia.

Huduma ya Kitaifa ya Polisi (NPS) yenye uwezo na usemi katika masuala ya matumizi ya pesa itaendeleza mtindo huu mkuu wa idara hiyo asipochukua hatua kubadilisha mtazamo wa maafisa wake ili waelewe kuwa wao ni watumishi na marafiki wa raia wanaofuata sheria ambazo wameajiriwa kulinda.

Hilo litafanyika iwapo uhuru wa kifedha utakumbusha mkuu wa polisi kuwa maafisa wake hawawezi kuvunja sheria ili kuilinda na hakuna sheria kama polisi wanavunja sheria. Kazi yao itakuwa ngumu kama raia hawaamini polisi na vituo vyao.

Kanuni moja ya utendakazi wa polisi iliyotayarishwa kwa ajili ya matumizi jijini London mnamo 1829, inawahitaji polisi "kutambua kuwa imani ya umma ni muhimu zaidi katika kufanikisha kazi yao. Wana jukumu la kujenga na kudumisha imani kutoka kwa raia ambao ndio wateja wao wakuu."

Heshima ni kuwili, lakini polisi hawataipata kutoka kwa raia wanawaochukulia kuwa maadui. Je, Makao Makuu ya Polisi hayaoni haja ya kutenga bajeti ya kufadhili mpango wa kutoa upya mafunzo kwa maafisa wake? Rais Ruto hajali? Wanafaa. Kwa sababu wote wanalipwa kwa pesa za umma.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

**Kanuni inayoongoza utendakazi wa maafisa wa polisi nchini Kenya ni kwamba raia ni adui. Kimsingi, maafisa hao ni watumisha wa huduma lakini kivitendo wanafana kazi kama kwa kutumia nguvu, aghalabu kupita kiasi. Wanalinda masilahi ya nchi na wenye mamlaka makuu huku wakihujumu na kudharua masilahi ya umma.**

Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

■ Mahasla hawataruhusu viongozi wachache kuchelewesha mageuzi ya kijamii na kiuchumi

# Ni lazima Ruto awe kielelezo ili kuwazima wabunge walafi



MACHARIA GAITHO

Si ajabu kwamba wabunge wameweka kando miegemeo yao ya kisiasa na kuungana kupigania nyongeza za mishahara na marupurupu. Kwa muda mrefu, imekuwa kawaida kwa wabunge kushughulikia maslahi yao binafsi, bila kujali shida za wananchi wanaowachagua.

Lakini kuna matumaini kwamba huenda mwelekeo huo ukabadilika, ikizingatiwa kuwa serikali mpya imekita msingi na utendakazi wake kwenye juhudi za kutetea watu maskini badala ya viongozi wachache.

Wabunge, ambao wameweka suala la nyongeza za mishahara na marupurupu kuwa la kwanza kujadiliwa Bunge likianza vikao vyake, watashangaa Rais Ruto, Hasla Mkuu wa Mahasla na Mwakilishi Mkuu wa wenye njaa, hasira na walionyanyaswa, akizima mpango wao.

Ikizingatiwa kwamba muungano wa Kenya Kwanza unajumuisha Chama cha Kikomunisti Kenya (CPK), Rais Ruto hatakubali hali ambapo viongozi wataendelea kujiongezea mishahara huku mamilioni ya raia wakiogelea katika umaskini. Kwa sasa, wanasiasa wa Kenya ni miongoni mwa viongozi wanaolipwa mishahara mikubwa sana duniani.

Wabunge wakiendelea na shinikizo zao, Kiongozi wa Mapinduzi ya Raia ataongoza Mahasla kwenye maandamano ya 'Kuvamia Bunge' Wabunge wote wa Kenya Kwanza ambao wameungana na wenzao wa Azimio kushinikiza nyongeza za mishahara yao, ni lazima waambiwe kuwa wao ndio wasaliti wa juhudi za ukombozi na hakuna asiyejua adhabu ya kosa la uhaini.

Muungano wa Kenya Kwanza ulichaguliwa kutokana na ajenda ya kujitolea kwake kupigania maslahi ya mwananchi. Mpango wake wa kiuchumi wa Bottom-Up hauwezi kufikiwa ikiwa walio uongozini wataanza kupigania maslahi yao binafsi.

Badala ya kulinda au kuongeza mishahara na marupurupu wanayolipwa wabunge na viongozi wengine wakuu serikalini, serikali ya Kenya Kwanza itageuza hali, ambapo uongozi utaonekana kuwa njia ya kuhudumia raia wala si jukwaa la viongozi kujitajirisha.

**Wabunge wakiendelea na shinikizo zao, Kiongozi wa Mapinduzi ya Raia ataongoza Mahasla kwenye maandamano ya 'Kuvamia Bunge' Wabunge wote wa Kenya Kwanza ambao wameungana na wenzao wa Azimio kushinikiza nyongeza za mishahara yao, ni lazima waambiwe kuwa wao ndio wasaliti wa juhudi za ukombozi na hakuna asiyejua adhabu ya kosa la uhaini.**



Wabunge wakiapishwa mnamo Septemba 8. Shughuli hiyo iliongozwa na Kaimu Karani wa Bunge la Kitaifa Serah Kioko. PICHA | JEFF ANGOTE

Kwa mantiki hiyo, Rais Ruto hatawaruhusu viongozi wa Kenya Kwanza; wakiwemo wabunge, magavana na mawaziri, kupokea mshahara unaozidi Sh60,000 kwa mwezi, ambao ni Kiwango cha Wastani kwa wafanyakazi wengi. Kutokana na majukumu mengi waliyo nayo baadhi ya viongozi, Rais atawaruhusu kulipwa marupurupu ya nyumba na usafiri yasiyopita Sh60,000 kwa mwezi.

Ni wazi kuwa Rais Ruto na Naibu Rais Rigathi Gachagua wataongoza kwa mfano kwa kupunguza mishahara na marupurupu yao.

Marupurupu wanayopokea kama yale ya nyumba, burudani, usafiri, wafanyakazi na usalama, pia yatapunguzwa kutokana na hali ngumu ya kiuchumi inayoikabili nchi.

Ili kuwa mfano bora, ni lazima viongozi wote; waliochaguliwa na walioteuliwa, waonyeshe kujitolea kutimiza ahadi zao kwa vitendo, kama walivyowaambia raia wakati wa kampeni.

Wao ndio wawakilishi wa maslahi ya mamilioni ya watu waliowachagua. Utakuwa usaliti mkubwa kwa wafuasi wao, iwapo watasahau majukumu yaliyowafanya watu hao kuwachagua.

Serikali ya 'Mahasla' haitakubali viongozi ambao lengo lao litakuwa tu kujitajirisha, sawa na familia maarufu tajiri zilizokuwa uongozini.

Kupunguzwa kwa mishahara ya viongozi kutakuwa mfano bora kwa nchi kupunguza matumizi ya fedha kwa masuala yasiyo muhimu.

Hatua hiyo pi itakuwa manufaa makubwa kwa nchi, kwani pesa hizo zitaelekezwa kwa masuala muhimu kama vile utekelezaji wa Hazina ya Mahasla.

Ni hatua itakayokuwa kama mwanzo wa kuleta usawa katika jamii na kupunguza pengo la kimapato kati ya maskini na matajiri.

Kampuni za kibinafsi na mashirika ya serikali yatashawishika kutathmini tena taratibu zinaotumia katika kuwalipa mishahara wafanyakazi wake.

Katika mashirika mengi, maafisa wanaoshikilia nafasi za juu hujilipa mishahara mikubwa, huku wakiwakandamiza wafanyakazi wa kiwango cha chini. Ikiwa wabunge hao watakaidi agizo la Rais Ruto kuhusu mishahara yao, lazima wajitayarishe kufurushwa nje ya Bunge.

Mwamko mpya wa 'Mahasla' haupaswi kuruhusu wabunge kadhaa kuzuia utimizaji wa malengo yake kuhusu mageuzi ya kiuchumi na kisiasa nchini.

Jeshi la 'Mahasla' linapasha misuli moto. Wabunge wasipobadilisha mpango wao watajua kwamba mapinduzi ya kiraia yaliyofanyika nchini Urusi, Ufaransa na Iran yalikuwa mfano tu. Huo ndio ujumbe ambao watu milioni saba waliompigia Rais Ruto kura wanamtarajia kuwapa wabunge.

Kama hatawakabili wabunge, yeye pia ataonekana kuwa msaliti wa Mapinduzi hayo na huenda yeye pia akawa kwenye hatari ya kung'olewa uongozini pamoja na wabunge hao. Mwamko huu mpya wa kisiasa haupaswi kuonekana kama njia ya kuhangaisha au kutishia familia ama watu matajiri.

Tangu uhuru, Kenya imekuwa ikitawaliwa na kundi la watu wachache waliowasaliti wapiganaji wa Mau Mau, wakawatenga maskini na kugeuza rasilimali za nchi kuwa mali yao binafsi. Lazima makundi hayo yasambaratishwe. Lazima wanyang'anywe mali yote ya nchi waliyonyakua ili wafahamu uchungu ambao watu maskini wamepitia.

Huu ni mwamko mpya wa watoto wa mashujaa wa Mau Mau. Lazima maadui wa mwamko huo mpya katika Bunge, Idara ya Mahakama, vyombo vya habari, mashirika ya kutetea haki za umma, polisi na mawakala wa nchi za kigeni waondolewe bila huruma.

Siku itakapowadia, hawatakuwa na mahali pa kujificha. Kama alivyoimba mwanamuziki Peter Tosh, "Wakandamizaji watatorokea baharini, lakini itakuwa ikichemka; watatorokea kwenye majabali, lakini yatakuwa yakiyeyuka."

***gaithomail@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ HAKUNA KUSTAAFU HIVI KARIBUNI

# WAKONGWE WA SIASA DAMU

*Baada ya kufurahia mamlaka, ushawishi na pesa nzuri kwa miongo kadhaa, wanaiasa wengi wakongwe sasa wamebadili mkondo kisiasa baada ya kukataliwa debeni mnamo Agosti 9.*

• Na OSCAR OBONYO

MNAMO Aprili mwaka jana, aliyekuwa Gavana wa Meru, Kiraitu Murungi, alieleza jinsi siasa ilimpokonya nafasi ya kuishi maisha yake. Wakati huo, Murungi alikuwa akiendelea kupata nafuu baada ya kuambukiza ugonjwa hatari wa Covid-19. Alimkejeli kiongozi wa ODM, Raila Odinga, aliposema kuwa, kwa mtazamo wake (Raila), siasa huja mbele ya afya yake.

"Nilitizama kwa huruma, Raila Odinga mdhaifu, ambaye alikuwa akitibiwa Covid-19, akitolewa kitandani ili aonekane pamoja na Rais Uhuru Kenyatta akizindua barabara katika kaunti za Nairobi na Kajiado. Hatua hii ililenga kutimiza malengo ya kisiasa," akaandika Bw Murungi katika makala magazetini huku akiapa "kujikomboa kutoka kwa minyonyoro ya kisiasa" na kuendeleza maisha yake binafsi.


Lakini, licha ya uchaguzi mkuu wa Agosti 9, kumpa Bw Murungi, 71, nafasi ya kustaafu na kurudi nyumbani kuishi maisha ya utulivu na familia yake, mwanasiasa huyo ameamua vinginevyo.

Baada ya kushindwa na Bi Kawira Mwangaza katika kinyang'anyiro cha ugavana, Murungi ameamua kuendelea na siasa kupitia mrengo wa Kenya Kwanza unaoongozwa na Rais William Ruto.


Murungi ni mfano wa mwanasiasa ambaye moyoni angetaka kustaafu lakini anavutwa nyuma na hamu ya mamlaka na hulka ya kusifu viongozi wakuu serikalini.

Alikuwa Mbunge wa Imenti Kusini kwa miongo miwili, Waziri kwa mwongo mmoja na mwongo mwingine akawa seneta na gavana. Kwa hivyo, kuondoka siasani hakujawa rahisi kwake sawa na wanasiasa wengine wakongwe.

Murungi ni mmoja wa wanasiasa hao wenye umri wa miaka 70 kwenda juu, ambao wameambukizwa "kirusi" cha siasa, na ambao licha ya kuwa mamlakani kwa miaka mingi, sasa wanasakata densi nyingine ya kisiasa baada ya kushindwa katika uchaguzi mkuu wa Agosti 9.



David Musila



Jimmy Angwenyi

Wengine ni aliyekuwa Gavana wa Makueni, Profesa Kivutha Kibwana, David Musila, aliyekuwa Waziri Msaidizi wa Uchukuzi, Chris Obure na aliyekuwa Mbunge wa Kitutu Chache Kusini, Jimmy Angwenyi.

Aliyekuwa Gavana wa Kisii, James Ongwae, ambaye aliongoza kampeni za Raila katika eneo la Nyanza, pia alihama Azimio na kujiunga na Kenya Kwanza.

Viongozi hawa walijiunga na Ruto baada ya kutangazwa mshindwa wa uchaguzi mkuu uliopita.

Wanasaisa wengi katika kundi hili la wakongwe ni magavana James Orengo (Siaya), Profesa Anyang'o (Kisumu) na Seneta wa Siaya, Dkt Oburu Oginga, ambaye ni kaka mkubwa wa Raila.

Watatu hawa, ambao ni washirika wakuu wa kiongozi huyo wa ODM, pia wamekuwa wakishinikizwa wastaafu.

Licha ya kuwania urais mara tano na kushindwa, Raila, 77, hajaonyesha dalili kwamba atastaafu siasa. Katika uchaguzi uliopita, wapinzani wake wa kisiasa walitumia suala la umri kuendesha kampeni dhidi yake.

Walidai umri wake mkubwa ungeathiri uwezo wa kutekeleza wajibu wake kama Rais.

Mtindo wa wanasiasa kubuni miungano ya kisiasa kuendeleza masilahi ya kibinafsi umechangia hali hii ya wanasiasa kuhama vyama vyao.

Bw Murungi ambaye, kwa mfano, ameshiriki kila uchaguzi kwa kutumia chama kipya cha kisaisa, tangu 1992, anashikilia rekodi ya kuhama vyama katika historia ya taifa hili.

Alikuwa Mbunge wa lililokuwa eneobunge la MeruKusini kwa tiketi ya Ford Kenya mnamo 1992.

Baadaye alihamia Democratic Party (DP), National Rainbow Coalition (NARC) chama cha The Party of National Unity (PNU) katika chaguzi za 1997, 2002 na 2007, mtawalia.

Murungi alichaguliwa Seneta wa Meru 2013 kwa tiketi ya chama cha Alliance Party of Kenya (APK), maarufu kama 'Bus' na baadaye Gavana 2017 kwa chama cha Jubilee.

Katika uchaguzi wa Agosti 9, alishiriki kwa chama kipya cha kisiasa cha Devolution Empowerment Party (DEP).

Rais Ruto na Raila ndio wamekaribia rekodi hii ya Murungi ya kuhama vyama.

Wawili hao wamebadili vyama vya kisiasa mara kumi, kila mmoja mara tano.

Ruto amekuwa mwanachama wa Kanu, ODM, United Republican Party (URP), Jubilee na United Democratic Alliance (UDA).

Naye Raila amewahi kuwa mwanachama wa Ford Kenya, National Development Party (NDP), Kanu, Liberal Democratic Party (LDP) na ODM.

Kwa mtazamo wake, Murungi anaelezea hatua hii ya kuhama vyama kuwa "kujijenga upya kisiasa" - kitendo ambacho kimemwezesha kudumu siasani kwa miaka mingi.

Msomi huyo wa Chuo Kikuu cha Havard, Amerika, anasema kuwa katika siasa za sasa, huduma kwa wananchi ni muhimu.

Wanasiasa wanahitaji kujipanga kila mwaka wa uchaguzi ili kuweza kushinda na kuendelea kufurahia mamlaka.

Hata hivyo, kuna baadhi ya wanasiasa ambao wanaheshimu umri wao na wamestaafu siasa baada ya kushindwa katika uchaguzi.

Mfano ni aliyekuwa Makamu wa Rais Moody Awori, aliyeshindwa na Dkt Paul Otuoma (Gavana wa Busia) katika uchaguzi mkuu wa 2007.

Awori alisema alipoteza kiti chake kutokana na msisimko dhidi ya rais wa zamani Mwai Kibaki, ambao ulivuma katika eneo hilo la magharibi mwa Kenya.

Katika kitabu chake, "Riding on a Tiger", Bw Awori anasema alikuwa ameamua kugombea mara ya

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

mwisho 2007.

Alitimiza ahadi hiyo kwa sababu baada ya kushindwa hakushiriki uchaguzi mwingine wala kuhamia chama kingine cha kisiasa.

Awori, 94, anasema alikatalia mbali shinikizo kutoka kwa Raila aendelee na siasa baada ya 2007.

Hata hivyo, alihakikishia wakazi wa Funyula kuwa ataendelea kuwahudumia kama kiongozi wao nje ya siasa. Awori, ambaye alistaafu siasa akiwa na umri wa miaka 79, anasema hatua ya watu kuhama vyama inachochewa na tamaa ya uongozi "si kuhudumia wananchi bali kujitajirisha"

Lakini huenda aliamua kustaafu siasa za kutafuta mali kwa sababu tayari yeye ni tajiri. Anamiliki biashara katika sekta mbalimbali za kiuchumi zikiwemo kampuni za Mareba Enterprise Ltd, na Mocian Ltd. Pia ni Mkurugenzi Mkuu wa biashara zingine zake na za familia yake.

Sababu hiyo pia inaweza kutumiwa kuelezea hatua ya aliyekuwa Mwanasheria Mkuu, marehemu Charles Njonjo kutoka katika siasa.


Njonjo aliwahi kuwa Mbunge wa Kikuyu na Waziri wa Haki na Masuala ya Kikatiba kabla ya kustaafu siasa 1990. Wakati huo alikuwa na umri wa miaka 70.

Alistaafu baada ya Tume ya Uchunguzi iliyoongozwa na Cecil Miller kumhusisha na jaribio la kupindua serikali ya Rais Daniel Moi mnamo 1982.

Njonjo alihisi kuwa alistaafu kutoka "mchezo mchafu wa siasa", alivyopenda kusema, kwa sababu alikuwa na mambo mengine ya kufanya.

Hadi kifo chake mnamo Januari 2022, akiwa na miaka 102, Njonjo alikuwa akisimamia biashara zake.

**Awori, 94, anasema alikatalia mbali shinikizo kutoka kwa Raila aendelee na siasa baada ya 2007 baada ya mvutano mkali kuhusu uchaguzi. Hata hivyo, alihakikishia wakazi wa Funyula kuwa ataendelea kuwahudumia kama kiongozi waonje ya Bunge.**


James Ongwae

Alipenda kusema: "Sitaacha kufanya kazi hadi siku na wakati ambao nitashindwa kuinua mguu wangu."

Mtindo wa wanasiasa kuhama chama kimoja hadi kingine umekuwa jambo la kawaida zaidi nyakati hizi kuliko ilivyokuwa zamani.

Kwa mfano, Profesa Kibwana, ambaye amejiunga na Ruto, alipata kibarua cha haraka kwa kushirikishwa miongoni mwa wanasheria wa UDA katika kesi ya kupinga ushindi wake (Ruto).

Majaji wa Mahakama ya Upeo, wakiongozwa na Jaji Mkuu Martha Koome, walitupilia mbali kesi hiyo na kuidhinisha wa Ruto.

Profesa huyo wa sheria amekuwa akibadili misimamo ya kisiasa mara kadhaa, na wakati mmoja alitangaza kuwa angegombea urais. Baadaye alijiondoa na kumuunga mkono Raila.

Aligombea kiti cha seneta Makueni lakini akashindwa na mwanasiasa mchanga, aliyekuwa Mbunge wa Makueni, Daniel Maanzo. Kibwana ambaye alikuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kati ya 1977 na 2002, alikuwa miongoni mwa watetezi wa mabadiliko ya uongozi nchini katika miaka ya 1980 na 1990.

Aliendeleza harakati hizo za mageuzi akiwa msemaji wa Baraza la Kitaifa Kuhusu Mageuzi (NCEC). Tangu alipojiunga na siasa za uchaguzi mnamo 2002 na kuchaguliwa Mbunge wa Makueni, Kibwana alihudumu kama Waziri wa Ardhi, Makao, Mazingira na Mali Asili.

Kwa upande wake, Bw Ongwae ana tajiriba kubwa kwani amehudumu serikalini kwa zaidi ya miongo mitatu. Alianza kama Mkuu wa Tarafa (DO), kisha afisa wa idara ya uhamiaji, mchanganuzi wa masuala ya usimamizi, Mkurugenzi wa Mpango wa Mabadiliko katika Utumishi wa Umma na Katibu katika Afisi ya Rais.

Kutokana na nafasi kubwa aliyoshikilia katika kampeni za Raila, Ongwae angepewa wadhifa mzuri katika serikali kama Azimio ingeshinda urais.

Bw Musila, ambaye alihudumu katika utawala wa mikoa kati ya 1970 na 1990, anaonekana kupata utulivu katika siasa.

Tangu alipojiunga na siasa za uchaguzi mnamo 1997, Musila, 79, aliyehudumu kama Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa, amebadilisha vyama mara kadhaa.

Amewahi kuhama chama cha Wiper mara mbili. Kwa hivyo, wengi walibashiri kuwa angehamia mrengo wa Ruto. Mnamo 2017, Musila ambaye aliwahi kuwa mwenyekiti wa Wiper, alihama chama hicho na kuwania ugavana wa Kitui kama mgombeaji wa kujitegemea. Alirudi Wiper baada ya kushindwa na Charity Ngilu wa chama cha Narc.

Kwa mara nyingine alitoka Wiper miezi michache kabla ya uchaguzi mkuu wa Agosti 9 na kujiunga na Jubilee.

Hata hivyo, wimbi la viongozi wakongwe kujiunga na mrengo wa Ruto halijafurahiwa na baadhi ya washirika wake.

Mbunge wa Nyaribari Chache, Zaheer Jhanda, ni miongoni mwa wanasiasa wa kwanza kupinga hatua hiyo akiwataja kuwa "watu wanaotaka kuvuna mahala ambako hawakupanda."

Hata hivyo, Ruto ametoa hakikisho kuwa ni waliomfanyia kampeni pekee ambao watapewa nafasi ya kwanza katika serikali yake.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

# Jinsi ambavyo Ruto alidhibiti mamlaka

...Kutoka Uk 8

Kibarua kikuu kiliachiwa Marende kuamua aliyefaa kupewa nafasi hiyo. Chama cha ODM kilikuwa na wabunge wengi kuiko PNU, chake Bw Kibaki kwa hivyo kilitarajia kuwa Marende angekiunga mkono.

Lakini wengi walishangaa alipokataa kuingizwa katika mivutano hiyo ya kisiasa. Alikataa kutoa uamuzi wowote na kuacha wazi nafasi hiyo.

Alijiteua kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Shughuli za Bunge hadi Kibaki na Raila waliposuluhisha tofauti zao. Marende alisifiwa sana kwa uamuzi huo uliozingatia umoja wa nchi, badala ya maslahi na miegemeo ya kisiasa. Sawa na ilivyokuwa kwa Marende, macho yote yatakuwa kwa Wetang'ula kuhusu hali ya sasa.

Lakini kuna tofauti. Marende suala lililomkabili Marende lilihusu wanachama wa muungano mmoja wa kisiasa. Suala la Wetang'ula ni la miungano miwili pinzani, kuhusu ni upi ulio na wabunge wengi. Ingawa Spika hatarajiwi kuegemea upande wowote kisiasa, wakati mwingine kauli hiyo huwa haizingatiwi.

Kinyume na Marende, Wetang'ula anaonekana kuwa upendeleo wazi wa kisiasa, hasa kwa jinsi amekuwa akimkosoa vikali Raila tangu alipjiondoka katika uliokuwa muungano wa NASA na kujiunga na Ruto. Alihama pamoja na kiongozi wa ANC, Musalia Mudavadi.

Ikizingatiwa alichaguliwa Spika kutokana na mkataba kati yake na Kenya Kwanza, inatarajiwa Wetang'ula atatumia nafasi hiyo kuendeleza ajenda za muungano huo. Inaaminika kuwa, kwa kushinikiza wabunge wa Kenya Kwanza

Kumchagua Wetang'ula, Ruto alitaka kuhakikisha amedhibiti mabunge hayo mawili. Aliweka hilo wazi kwenye kikao cha wabunge wa Kenya Kwanza mjini Naivasha wikendi iliyopita. Ni mkakati huo huo, ambao uliwezesha muungano huo kutwaa nafasi ya Mwenyekiti wa Baraza la Magavana (CoG), kupitia Gavana Anne Waiguru wa Kirinyaga.

Kutokana za Rais Ruto kudhibiti Bunge la Kitaifa, Wetang'ula atakuwa mstari wa mbele kuhakikisha mipango yote ya Kenya Kwanza imefaulu.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Nation Media Group "ePaper Copy"

## SAYANSI NA TEKINOLOJIA



Elon Musk

# SpaceX inataka kupeleka setilaiti ya intaneti Iran


Kampuni ya SpaceX, itaomba iondolewe katika vikwazo ambavyo Amerika imewekea Iran katika juhudi za kutoa huduma za intaneti kupitia setilaiti nchini humo, mwenye kampuni hiyo, Elon Musk amesema.

"Starlink itaomba iondolewe katika vikwazo dhidi ya Iran," Musk akasema akijibu ujumbe wa Twitter kutoka kwa ripota wa masuala ya sayasi. Awali, Musk alikuwa amesema huduma za intaneti kupitia setilaiti zinapatikana katika kila bara - "ikiwemo Antarctica" - huku kampuni yake ikipanga kuzindua setilaiti 42,000 kuimarisha huduma za intaneti.

Mwanahabari wa sayansi, Erfan Kasraie, ambaye ni mzaliwa wa Iran, alikuwa amesema kupitia Twitter kuwa kupeleka huduma hizo Iran "kungeleta mabadiliko halisi ya siku zijazo" nchini humo, kauli iliyofanya Musk kumjibu.

Starlink, iliyoanzishwa 2020, inatoa huduma za intaneti yenye kasi kwa wateja katika maeneo yasiyo na mitandao ya simu za nyaya kupitia kundi la setilaiti kadhaa zinazozunguka ardhi kwa karibu.— *AFP*

# AJABU YA PETE ZA ZOHALI




**Mchoro wa mfumo wa jua, zikiwemo sayari nane na jua. Chini: Sayari ya Zohari, mnamo Juni 20, 2019, ilipokaribia Ardhi sana katika umbali wa kilomita bilioni 1.36.** PICHA | AFP

WASHINGTON

Pete zinazozunguka sayari ya Zohali (Saturn) ambazo zilivumbuliwa na Galileo miaka 400 iliyopita ni vitu vya ajabu ambavyo wanajimu wengi walio na darubini ndogo wanaweza kuona katika mfumo wa jua.

Lakini hata leo, wataalamu hawawezi kukubaliana jinsi zilivyoundwa. Utafiti mpya uliochapishwa katika jarida maarufu la sayansi unalenga kutoa jibu la kuaminika.

Kati ya miaka 100 na 200 milioni iliyopita, mwezi wenye barafu waliouita Chrysalis, ulivunjika baada ya kufika karibu na sayari hiyo kubwa yenye gesi, wanasema. Japo sehemu yake kubwa iligongana na Zohali, vipande vilivyobaki vilivunjika kuwa barafu ndogo na kuunda pete zinazoonekana katika sayari hiyo.

"Ni vizuri kupata maelezo ya kuaminika," akasema Jack Wisdom, profesa wa sayansi ya sayari katika Taasisi ya Tekinolojia ya Massachusetts (MIT) na kiongozi wa utafiti huo mpya.

Zohali, ambayo ndiyo sayari ya sita kutoka kwa Jua, iliundwa miaka bilioni nne na nusu iliyopita, mwanzoni mwa mfumo



wa jua. Lakini miongo michache iliyopita, wanasayansi walisema pete hizo zilitokea baadaye; yapata miaka 100 milioni iliyopita.

Dhana hii ilitiwa nguvu na ripoti iliyotolewa na Cassini, chombo ambacho kilizunguka Zohali kutoka 2004 hadi 2017.

"Lakini kwa sababu hakuna aliyeweza kufikiria njia ya kutengeneza pete hizo miaka 100 milioni iliyopita, baadhi ya watu wamekuwa wakiuliza sababu zilizofanya uamuzi huo kufikiwa," akasema Wisdom.

Kwa kuunganisha miundo kadhaa ya hesabu, Wisdom na wenzake walipata maelezo ambayo yalihalalisha muda, na kuwawezesha kuelewa vyema kitu kingine kuhusu sayari hiyo - kuinama kwake. Zohali imeinama kwa digrii 26.7. Ikiwa imejaa gesi, ilitarajiwa kuwa mchakato wa kuundwa kwake kungeizuia kuinama.

Majuzi , wanasayansi waligundua kwamba Titan, mwezi mkubwa kati ya miezi 83 ya Zohali, unahama kutoka sayari hiyo, kwa kiwango cha sentimita 11 kwa mwaka. Hii inabadilisha kiwango cha mhimili ambao inainamia.

Fikiria kuhusu kuzunguka juu ukichora duara. Karibu miaka bilioni moja iliyopita, mawimbi haya ya mtetemeko yalikutana na mzunguko wa Neptun, na kuunda mvuto wenye nguvu za smaku. Ili kudumisha hali hii, Titan ilipoendelea kutoka nje, ilibidi Zohali iiname, wanasayansi walieleza.

Lakini maelezo haya yalihusu kufahamu jinsi sayari hiyo iliundwa kwa ndani na sio nje au katikati.

Katika utafiti huo mpya, Wisdom na wenzake waliunda mfano wa ndani ya sayari hiyo kwa kutumia nguvu za data zilizokusanywa na Cassini wakati ilipoikaribia sana katika mzunguko wake wa mwisho kabla ya kutumbukia ndani ya Zohali.

— *AFP*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya Afrika

■ WASIWASI TELE KATIKA TAIFA HILO MAARUFU




Wafuasi wa chama tawala cha All Progressives Congress, wakisherehekea ushindi wa Rais Mohammadu Buhari jijini Abuja mnamo Februari 26, 2019. Taifa hilo maarufu zaidi Afrika litafanya uchaguzi mkuu chini ya miezi mitano ijayo katika kile kinachoonekana kuwa mtihani mkubwa wa umoja na uthabiti tangu mapinduzi ya kijeshi na utawala wa kidikteta katika miaka ishirini iliyopita. PICHA | AFP

# NIGERIA TUMBOJOTO

*Barabara ya kuelekea uchaguzi wa Februari inaonekana kuwa na vikwazo tele ukiwemo ukiukaji wa sheria, siasa za kikabila, majimbo kutaka kujitenga, uchumi kudorora na ukosefu wa imani katika taasisi za serikari, yote haya yakitishia kusambaratisha taifa hilo. Kuna ongezeko la majeshi ya waasi kaskazini mashariki, majangili, kaskazini magharibi na kati, wanamgambo eneo la kusini, wapiganaji wanaotaka kujitenga kusini mashariki*

● NA MOHAMMED MOMOH AND HARRY MISIKO

Nigeria, nchi yenye watu wengi zaidi Afrika, itafanya uchaguzi mkuu chini ya miezi mitano ijayo, katika kile kinachoonekana kuwa mtihani mkubwa kwa umoja na uthabiti wa nchi hiyo tangu mwisho wa mapinduzi ya kijeshi na udikteta miongo miwili iliyopita.

Barabara ya kuelekea uchaguzi wa Februari inaonekana kuwa yenye matuta mengi kwa kila hali kukiwa na mseto wa ukiukaji wa sheria, siasa za kikabila, majimbo kutaka kujitenga, uchumi unaodorora na ukosefu wa imani katika taasisi za serikari, yote haya yakitishia kusambaratisha nchi hiyo ya Afrika Magharibi.

Idara za usalama za nchi hiyo, tume ya uchaguzi, mahakama na mfumo wa kidini ziko kwenye mitihani huku zikitishiwa kuvurugwa. Nchi hiyo yenye uchumi thabiti barani Afrika imejipata katika hali ambayo wachanganuzi wa serikali na usalama wanasema inaweza kulinganishwa na yaliyotokea kabla ya vita vya ndani vya 1967 hadi 1970.

Kuna ongezeko la majeshi ya waasi Kaskazini Mashariki, majangili upande wa Kaskazini Magharibi na Kaskazini ya Kati, wanamgambo eneo la Kusini, wapiganaji wanaotaka kujitenga upande wa Kusini Mashariki na wauaji wa kutoa matambiko Kusini Magharibi.

Ghasia zilizopangwa zinaendelea kote katika nchi hiyo kubwa na kutimua wanaoweza kuwa wapigakura makwao na kuvuruga mipango ya Tume Huru ya Kitaifa ya Uchaguzi (INEC) — ikiwemo kuchomwa kwa afisi zake, kuuawa kwa maafisa wa uchaguzi na kuchomwa kwa vifaa vya uchaguzi.

Katika eneo la Kaskazini Mashariki, watu zaidi ya 60,000 wameuawa na wengine zaidi ya 2.2 milioni kufurushwa makwao tangu 2009 katika mapigano yanayotekelezwa na makundi ya Boko Haram na Islamic State of West Africa Province (ISWAP).

Katika eneo la Kaskazini ya Kati na Kaskazini Magharibi, majangili wasiotambuliwa wanaendelea kuua na kujeruhi bila kukabiliwa huku makundi yanayotaka kujitenga yakizua ghasia na kudhibiti eneo la Mashariki na jimbo la Niger Delta wakiapa kusimamisha uchaguzi katika majimbo tisa - Abia, Akwa-Ibom, Bayelsa, Cross River, Delta, Edo, Imo, Ondo na Rivers.

Miongoni mwa makundi yanayoende-

...Endelea Uk 26

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya Afrika

# Hofu yazidi Nigeria ikikaribia uchaguzi mkuu

...Kutoka Uk 25




Afisa wa polisi akilinda lango la kituo cha kupigia kura katika Jimbo la Rivers. mjini Port Harcourt, Kusini mwa Nigeria mnamo Februari 26, 2019, wakati wa uchaguzi.

leza kampeni ya kujitenga huku yakimwaga damu ni Indigenous People of Biafra (IPOB) ambalo kiongozi wake, Nnamdi Kanu, mwenye umri wa miaka 54, kwa wakati huu anakabiliwa na mashtaka ya vitendo vya ugaidi na uhaini kufuatia kukamatwa kwake jijini Nairobi mnamo 2021 na kurudishwa Nigeria.

Kundi lake la wanamgambo, Eastern Security Network (ESN), linaendelea kushambulia maafisa wa usalama na raia linalochukulia kuwa "wasaliti" katika majimbo matano ya Mashariki ya Anambra, Imo, Enugu, Ebonyi na Abia. Kulingana na ripoti ya SB Morgen, kundi la habari za kijasusi kuhusu siasa za Nigeria, nchi ilipoteza maafisa wa usalama wasiopungua 964 wakiwemo maafisa wa polisi 322 na wanajeshi 642 , katika mashambulizi ya magaidi, majangili na makundi yanayotaka kujitenga mwaka wa 2021.

Mnamo 2022, waziri wa Habari, Lai Mohammed alifichua kwamba ESN liliua maafisa 115 wa usalama kufikia Agosti.

Ghasia hizo zinachochewa na masuala kadhaa - ikiwemo dhuluma za kihistoria, kutengwa, azima za kujitawala, ukosefu mkubwa wa ajira na kupanda kwa gharama ya maisha, ambako kumeacha raia zaidi ya 100 milioni wakihangaika.

Kiwango cha mfumko kwa mwaka kiliongezeka hadi asilimia 19.64 Julai 2022, kikiwa cha juu zaidi tangu Septemba 2005, huku kupanda kwa bei za mkate, nafaka na viazi kukiathiri vibaya watu masikini.

INEC imeonya kuwa kuongezeka kwa ghasia, hasa uchomaji wa afisi zake na kuharibiwa kwa vifaa vya uchaguzi, kunaweza kuvuruga maandalizi, ukiwemo usajili wa wapigakura.

Mwenyekiti wa INEC Mahmood Yakubu anasema mashambulizi katika mali ya tume kunaweza kuharibu uwezo wao wa kuandaa uchaguzi na pia kuwa na athari mbaya kwa shughuli ya uchaguzi nchini humo.

**Nchi hiyo yenye uchumi thabiti barani Afrika imejipata katika hali ambayo wachanganuzi wa serikali na usalama wanasema inaweza kulinganishwa na yaliyotokea kabla ya vita vya ndani vya 1967 hadi 1970.**

Kulingana na ripoti rasmi, ofisi 41 za INEC zimechomwa au kuharibiwa kote Nigeria na watu walio na silaha wasio maafisa wa serikali katika miaka miwili iliyopita. "Haya ni mashambulizi yanayohusiana na ghasia za uchaguzi, malalamishi yasiyohusu uchaguzi na vitendo vya wahalifu na watu walio na silaha wasiojulikana," anasema Profesa Yakubu.

Wapigakura zaidi ya 95 milioni waliosajiliwa katika nchi hiyo iliyo na watu 218 milioni wanatarajiwa kuchagua rais mpya katika uchaguzi wa sita wa urais tangu Nigeria iliporudisha demokrasia mwaka wa 1999.

Mbali na rais, wapigakura pia watachagua magavana wapya, maseneta na wanachama wa Bunge la Wawakilishi na wabunge wa majimbo katika vituo 176,846 vya kupigia kura kati ya Februari 25 na Machi 2023.

Watu 14 wanagombea urais kumrithi Rais Muhammadu Buhari, 78, jenerali mstaafu wa jeshi ambaye ataondoka mamlakani baada ya mihula miwilli ya miaka minane.

Aliyekuwa Gavana wa Lagos na kiongozi wa chama tawala cha All Progressives Congress (APC), Bola Ahmed Tinubu, 70, aliyekuwa makamu rais mara mbili, Atiku Abubakar, 75, wa chama kilichotawala People's Democratic Party (PDP); na Peter Obi wa Labour Party (LP) ndio wagombeaji wakuu. Wengine ni Osita Nnadi (Action Peoples Party), Kolawole Abiola (Peoples Redemption Party), Yabagi Sani (Action Democratic Party) na Ado-Ibrahim Abdulmalik wa Young Progressives Party.

Wagombeaji wakuu wanatoka mfumo wa zamani wa majimbo na makabila wa Nigeria na hivyo kufanya uchaguzi huo kuwa unajikita katika misingi ya kikabila, chanzo cha ghasia na tisho kwa amani na umoja wa kitaifa.

**Wachanganuzi wamesema kuwa bila mamlaka, chama tawala kitakufa. Kiliundwa 2014 kutwaa mamlaka ya kisiasa kutoka kwa PDP.**

Nkasi Wodu, afisa mkuu wa Taasisi ya Aspen

Tinubu ni wa kabila la Yoruba kutoka Kusini Magharibi, Abubakar, ni Fulani kutoka Kaskazini na Obi ni Igbo kutoka Kusini Mashariki, huku kila jimbo, likitaka mwana wao kuingia ikulu ya rais jijini Abuja.

Uwezekano wa ghasia za uchaguzi unanukia, anasema Nkasi Wodu, wakili na mhadhiri mkuu chuo cha Aspen Institute, hasa kati ya vyama viwili vikuu vya kisiasa ambavyo vinapigania ubabe vikikabiliwa na changamoto tofauti.

"Wachanganuzi wamesema kuwa bila mamlaka, chama tawala cha APC, kilichoundwa 2014 kutwaa mamlaka ya kisiasa kutoka kwa PDP, kinaweza kusambaratika, ilhali kushindwa kwa PDP katika uchaguzi wa urais kwa mara ya tatu 2023 kunaweza kukimaliza. Ni kwa sababu hiyo ambapo uchaguzi huo unatarajiwa kuwa na ushindani mkali," wakili huyo mtaalamu wa masuala ya kujenga amani Afrika aliandika katika ripoti ya Fragile States Index.

Huku Tinubu akigombea kwa tikiti ya chama kinachotawala, Abubakar aliyegombea urais kwa zaidi ya mara nne, anategemea sifa zake kama makamu rais wa zamani, huku Obi, aliyeshindwa katika azima yake ya kuwa makamu rais 2019, akiweka matumaini yake kwa vijana na kura za Wakristo - makundi ambayo yalihisi yalipuuzwa katika uteuzi wa APC na PDP.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya dunia

■ KUTA 'ZILIZOJAA MACHUNGU'

# SELI ZA MATESO ZA URUSI

*Akiwa ameketi ndani ya wadi moja katika hospitali kuu jijini -iliyoharibiwa vibaya na mashambulio ya mabomu - mfungwa anaelezea dhuluma alizopitia:kuchomwa kwa stima, kucharazwa mijeledi, kuvunjwa mifupa na kudungwa kwa sindano. Mkono wake wa kulia umewekwa bandeji na kufungiwa shingoni kwa mkanda. Amechoka lakini sauti yake ingali thabiti*



**Mykhailo Ivanovych akitembelea kituo cha polisi kilichoharibiwa mjini Izyum, mashariki mwa Ukraine, mnamo Septemba 18. Katika miji iliyokombolewa na majeshi ya Ukraine majuzi, habari zimetokea kuhusu kukamatwa, kuzuiliwa na kuteswa kwa wakazi. Akiwa hospitalini Izyum, Mykhailo ameanza kutembea tena. Mkono wake uliofungwa bandeji na kuning'inizwa shingoni kwa mkanda unauma na kumkumbusha kuwepo kwa wanajeshi wa Urusi mjini humo.** PICHA | AFP

• KYIV

Kwa wanaozuiliwa katika seli za chini ya ardhi katika gereza moja la muda linalosimamiwa na Urusi mjini Izyum, Ukraine, kulikuwa na zaidi ya aina moja ya mateso. Wavamizi hao walitekeleza aina tofauti za matesodhidi ya waliozuiliwa katika gereza hilo.

Mykhailo Ivanovych, 67, anasema alipitia nyingi za mateso hayo.

Akiwa ameketi ndani ya wadi moja katika hospitali kuu ya mjini humo - iliyoharibiwa vibaya na mashambulio ya mabomu - mfungwa huyu anaelezea mateso aliyopitia: kuchomwa kwa stima, kucharazwa mijeledi, kuvunjwa mifupa na kudungwa kwa sindano. Mkono wake wa kulia umewekwa bandeji na kufungiwa shingoni kwa mkanda. Amechoka lakini sauti yake ingali thabiti.

"Walinitesa kwa siku 12," anasema. "Walinicharaza mijeledi kila mahali. Walivunja mkono wangu. Mrusi mmoja alikuwa ameishikilia huku mwenzake akiichara. Walinicharaza hadi wakati ambapo mwili wangu uliganda na singehisi uchungu. Walichoma kucha zangu kwa kutumia nyaya zenye nguvu za umeme - zilichomeka vibaya."

Kisha walinidunga kwa sindano mara kadhaa mgongoni. Sindano hizo zilikuwa ndefu sana na walishindilia zote ndani ya ngozi yangu."

Hiyo ilikuwa Septemba 11, wanajeshi wa Ukraine walipoingia kwa nguvu mjini humo. Hatua hiyo ilikomesha utawala wa Urusi mjini humo. Baada ya kuteka mji huo, wanajeshi wa Urusi waliutumia kama ngome ya kutekeleza mashambulio katika eneo la mashariki mwa Donbas. Pia walitumia mji huo kama kituo cha kuhifadhi silaha, vifaa na mahitaji mengine ya kivita.

Mykhailo alizuiliwa pamoja na wenzake ambao Urusi ilishuku wangevuruga mipango yao. Waalifunikwa nyuso na kuzuiliwa katika seli chafu ambako walitendewa kila aina ya mateso. "Wote tuliozuiliwa pamoja waliteswa kinyama," anasema. "Nyakati fulani baadhi ya watu waliondolewa kutoka seli wakiwa hali mbaya. Nilimuona mmoja ambaye nilidhani alikufa."

Mykhailo amevalia rozari shingoni na tishati ya manjano. Nauliza iwapo aliomba kwa muda ambao alikuwa katika seli hizo. "Ndio", anajibu. "Nililazimika kuomba. Mtu mwingine pia angeomba akiwa humo,"

...Endelea Uk 28

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kirunzi ya dunia

# ‘Vyumba vya mateso’ vya Urusi nchini Ukraine



Wapelelezi wabeba mfuko wa maiti kutoka kwa kaburi la halaiki ndani ya msitu nje ya mji wa Izyum, mashariki mwa Ukraine, Septemba 18. Maafisa wa serikali ya Ukraine wamepata makaburi 450 nje ya mji wa Izyum, uliokuwa umetekwa na Urusi, huku baadhi ya maiti zilizofukuliwa zikiwa na alama za mateso.

...Kutoka Uk 27

Mateso hayo yalitekelezwa katika kituo cha polisi mjini Izyum. Kilikuwa hali mbaya tulipoingia. Baadhi ya milango haikuwepo na madirisha yalikuwa yameharibiwa na upepo.

Sawa na sehemu nyingi mjini Izyum, kituo hicho cha polisi kilishambuliwa na wanajeshi wa Urusi kabla yao kuteka mji huo.

Giza linatanda tunapoteremka kwenye ngazi za seli hizo zilizo katika orofa mbili chini ya ardhi. Nyingi ni ndogo na chafu huku vipande vya nguo vikitumika kama malazi. Katika seli moja, mtu amechora laini kadhaa ukutani kuashiria muda ambao amefungiwa humo.

Hali ya utulivu inavurugwa na mwanajeshi wa Ukraine. “Inaonekana kuwa kuta hizi zinaashiria machungu na mahangaiko,” anasema.

Masimulizi ya Mykhailo kuhusu alivyoumizwa kwa stima yanafanana na mengine tuyosikia hivi majuzi katika maeneo yaliyokombolewa na wanajeshi wa Ukraine kutoka kwa Urusi.

**Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky anasema “vyumba 10 vya mateso” vimepatikana siku za hivi majuzi katika maeneo ya jimbo la Kharkiv ambalo limekombolewa na majeshi ya Ukraine.**

Tulisikiza ushuhuda mwingine kutoka kwa mwanahabari wa zamani kwa jina Maxim, aliyesema alizuiliwa katika seli hizo hizo. “Wanaweka stima tayari na unaanza kutetemeka,” anasema. “Nilikuwa nikianguka kutoka kwa kiti kwa uchungu. Giza lilikuwa totoro.”

Ukraine inataka kuthibitisha kuwa mateso dhidi ya raia wake ni uhalifu wa kivita na yalipangwa. Kwamba hayakutekelezwa kwa sadfa.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky anasema “vyumba 10 vya mateso” vimepatikana siku za hivi karibuni katika maeneo kadhaa ya mkoa wa Kharkiv, ambao umekombolewa na wanajeshi wa Ukraine.

Hatua chache kutoka gereza hilo, tunawapata wapelelezi wakiendelea na kazi. Wanachakura vifusi katika jengo la afisi lililoharibiwa na ambalo lilikuwa likitumiwa na wanajeshi wa Urusi kama kituo cha kupanga mashambulio.

Tunaruhusiwa kuingia ndani tukiwa tumevalia vifaa vya kukinga viatu vyetu na barakoa ili tusivuruge ushahidi. Kibao chenye jina “Polisi”, kwa lugha ya Kirusi, bado kinaning’inia juu ya mlango.

Ndani, juu ya dawati kuna toleo la gazeti la kila siku la Urusi. Kiongozi wa upelelezi, Leonid Pustovit – akiwa amevalia kabuti jeupe - amegundua ushahidi wa kushangaza.

Anafungua kabati moja kutuonyesha shoka moja lenye alama za kile kinachofanana na damu. “Uchunguzi wetu utafichua hii ni damu ya nani,” anatwambia. Anapata pia hati yenye orodha ya majina ya watu ambao Warusi walishuku wanaunga mkono serikali ya Ukraine. Hati hiyo ilikuwa imehifadhiwa na wanavamizi hao. “Watu hao walichukuliwa kuwa wenye misimamo mikali,” anasema. “Wanajeshi wa Urusi waliwaleta hapa kuwahoji,” anaongeza.

**Wanaweka stima tayari na unaanza kutetemeka,” anasema. “Nilikuwa nikianguka kutoka kwa kiti kwa uchungu. Giza likuwa totoro**

Maxim, mwanahabari

Mji huu ulioharibiwa unaanza kuelezea maovu ambayo wanajeshi wa Urusi walitenda na kufichua idadi ya waathiriwa wa mateso mikononi mwa Warusi.

Katika msitu mmoja viungani mwa mji, wapelelezi wanaendelea kufukua mabaki ya watu waliozikwa katika zaidi ya makaburi 440. Maafisa wa utawala wanasema wengi wa watu hao ni raia.

Hata hivyo, kaburi moja lina maiti za wanajeshi 17. Baadhi yao walizikwa mikono ikiwa imefungwa, ishara ya mateso waliyopita kabla ya kufa.

Mkuu wa usalama katika eneo hilo anasema wanajeshi wa Urusi ndio walioua wote waliozikwa hapa. Waliwaua kwa kuwapiga risasi, mabomu na mashambulio kutoka angani.

Huku wafanyakazi wa shirika moja la uokoaji wakibeba mabaki hayo ndani ya mfuko mweupe unaotumika kubebea maiti, Olena Kazabekhov, anatazama akiwa na hisia mseto.

Mwanamke huyo amefika hapo kutafuta mabaki ya baba yake, Petro Vasylchyshyn, aliyehudumu katika kikosi cha wanajeshi wa Ukraine kwa jina, “95th Airborne Battalion”. Amejawa na huzuni huku akifarijiwa na mumewe, Yurii, aliyeandamana naye.

“Tulizungumza kwa simu mara ya mwisho Aprili 17,” anatueleza. “Siku iliyofuata walienda vitani na baadhi ya wenzake hawakujulikana waliko. Tunajua watano waliuawa. Maiti zao zilipatikana na mwenzao mmoja.

Huku akihangaishwa na maswali mengi yasiyo na majibu, Yurii anasema wao pia wanatamani kupata mabaki ya Petro wakayazike.

“Tunajua familia ambazo zilikuwa katika hali yetu sasa lakini walipata miili ya wapendwa wao. Angalau wanafurahi kwamba wamepata mabaki ya kuzika.”

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

■ WAWANIAJI BRAZIL WAPELEKA VITA VYA HABARI KATIKA TV

# UONGO MTUPU

*Televisheni inaeneza zaidi uongo ambao umekuwa ukiendelea kwa miezi kadhaa katika mitandao ya kijamii huku taifa likijiandaa kwa uchaguzi mkuu mwezi ujao*

● RIO DE JANEIRO

Habari za kupotosha katika mitandao ya kijamii zimekuwa jambo la kawaida huku Brazil ikielekea katika uchaguzi ambao umezua migawanyiko mikubwa. Lakini habari hizo zinaweza kuvutia na kufikia watu wengi zikitoka moja kwa moja kwa wagombeaji katika televisheni ya taifa.

Kuanza rasmi kwa kampeni za uchaguzi mkuu wa Oktoba 2 kunamaanisha wagombeaji wanaweza kutumia TV, yakiwemo mahojiano, midahalo na matangazo ya kila siku yanayolipiwa kwa pesa za umma.

Hiyo inamaanisha kufurika kwa habari feki nchini Brazil, iwe ni kuhusu rais aliye mamlakani, Jair Bolsonaro na mpango wake wa kubuni mfumo wa malipo wa "Pix", au mgombeaji mkuu Luiz Inacio Lula da Silva kudai aliondolewa mashtaka yote ya ufisadi yaliyomkabili, kama mfano kama mfano.

Ukweli wa mambo ni kuwa, Benki Kuu ya Brazil ilianza mpango wa Pix mwaka wa 2018, mwaka mmoja kabla ya Bolsonaro kuingia mamlakani. Na Lula, aliyeongoza Brazil kutoka 2003 hadi 2010, aliondolewa vifungo vyake jela kuhusu kashfa za ufisadi kwa misingi ya utaratibu. Hakuondolewa lawama.

"Kampeni ni zaidi ya kila aina ya vita vya masimulizi," na wagombeaji hutumia taarifa za za kupotosha au za uongo kujipigia debe, anasema Amaro Grassi, mtaalamu wa sera ya umma katika Wakfu wa Getulio Vargas Foundation. Hakuna jambo geni kuhusu uongo katika siasa.

Lakini wachanganuzi wanaonya kuwa televisheni sasa inaeneza kwa mapana zaidi habari za kupotosha ambazo zimekuwa zikiendelea kwa miezi kadhaa katika mitandao ya kijamii nchini Brazil. "Televisheni bado inawapa habari watu wengi" nchini Brazil, anasema Arthur Ituassu, Profesa Mwandamizi wa mawasiliano ya siasa katika Chuo Kikuu ch Pontifical Catholic University, jijini Rio de Janeiro.

Tofauti na mitandao ya kijamii, runinga za Brazil - ambako watu wengi bado wanatazama vituo vikubwa vichache, hasa TV Globo - zinafikia watu wengi," anasema.

"Televisheni bado inafikia umma kwa jumla, zaidi ya watu ambao tayari wako katika mrengo mmoja au mwingine," anasema Helena Martins, profesa wa mawasiliano katika Chuo Kikuu cha Federal University of Ceara. Pia, watu wengi wanaamini "kama hakijaonekana kwa TV, basi si cha kweli," anaongeza.

Uchaguzi wa 2018, ambao Bolsonaro alishinda, ulikuwa umejaa habari za kupotosha, hasa katika mitandao ya kijamii - ambayo ina nguvu katika nchi hiyo iliyo na simu nyingi za kisasa kuliko watu (zinakadiriwa kuwa 242 milioni, dhidi ya watu 213 milioni). Kampeni za wakati huu ni chafu zaidi, ikizingatiwa kuwa uchaguzi wa urais umechacha sana kati ya rais aliye mamlakani mwenye msimamo mkali na hasimu wake anayekumbatia mageuzi.

Katika migawanyiko hiyo mikubwa, asilimia 85 ya raia wa Brazil wanasema habari za kupotosha zinaweza kuathiri vibya matokeo ya uchaguzi, kulingana na kura ya maoni ya taasisi ya Ipec, iliyochapishwa Septemba 6.

Hata hivyo, kura za maoni zinaonyesha ni wapigakura wachache sana ambao hawajaamua. Asilimia 78 wanasema wamefanya uamuzi wa mwisho, unaeleza utafiti wa taasisi ya Datafolha uliochapishwa wiki jana.

Utafiti huo ulionyesha kuwa Lula ana umaarufu wa asilimia 45 huku Bolsonaro akifuata kwa asilimia 33 - sawa na ilivyoonyesha kura ya maoni ya awali ya taasisi hiyo.

Wagombeaji wengine walikuwa na umaarufu wa chini ya asilimia kumi. "Kuna kiwango cha juu sana cha kudumisha wapigakura. Hii inafanya vigumu kwa habari zozote kubadilisha hali wakati huu," akasema Grassi.

Lakini hali hiyo haijafanya wagombeaji kukoma kueneza habari za kupotosha katika ngome zao, wakitarajia kushawishi wapigakura wachache ambao hawajaamua.

Kwa mfano, Lula amekuwa akirudia kuongeza chumvi mafanikio yake katika uchumi. Naye Bolsonaro amekuwa akilaumu Lula kwa kupinga uenezaji injili na kuchukia kilimo biashara, makundi mawili yenye nguvu ambayo yanamuunga mkono kiongozi huyo aliye mamlakani.

"Lengo ni kuhimiza makundi hayo yaendelee kumkataa mpinzani wake." Anasema Grassi. "Kwa sababu katika uchaguzi wenye ushindani mkali kama huu, unaishia kuwa vita vya kukatalia."

— *AFP*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

**Uchaguzi wa 2018, ambao Bolsonaro alishinda, ulikuwa umejaa habari za kupotosha, hasa katika mitandao ya kijamii - ambayo ina nguvu katika nchi hiyo iliyo na simu nyingi za kisasa kuliko watu (zinakadiriwa kuwa 242 milioni, dhidi ya watu 213 milioni).**



**Mgombea urais wa Brazil kwa chama cha Workers Party, Luiz Inacio Lula da Silva, akihutubia mkutano wa kampeni mjini Porto Alegre mnamo Septemba 16. Kampeni hizo zilizoanza rasmi mwezi uliopita kabla ya uchaguzi wa Oktoba 2, zitawapa wagombea nafasi kubwa ya kujipigia debe kupitia kwa TV, ikiwemo katika habari kuu, mahojiano, mijadala na matangazo ya kila siku yanayolipiwa kwa pesa za uuma.** PICHA | AFP

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

TANZIA

■ MKONGWE WA VITA VYA UHURU

# MAU MAU WA BUSIA AAGA

*Akiwa mwenyekiti wa vuguvugu la Kavirondo tawi la Busia, Chifu wa zamani Wanga Mahanga Oniang' alikusanya pesa zilizotumiwa kutengeneza bunduki nyumbani na kuwapelekea chakula wapiganaji wa Mau Mau*

● NA OSCAR OBONYO

KARIBU kilomita 457 magharibi mwa mji wa Nyeri, ambao ulikuwa kitovu cha vita vya kupigania uhuru vya Mau Mau miaka ya 1950, ndiko unapatikana mji wa Mau Mau, eneobunge la Budalang'i, Kaunti ya Busia.

Mmoja wa mashujaa wa vita vya uhuru kutoka mji huo alizikwa siku chache zilizopita. Chifu wa zamani, Wanga Mahanga Oniang', aliyekuwa miongoni mwa watu walioongoza harakati za kuwakabili Waingereza, alifariki siku chache kabla ya Malkia Elizabeth II wa Uingereza.

Ajabu ni kuwa, Malkia alifariki siku ambayo Mzee Mahanga alizikwa, sadfa inayowashangaza watu wengi wa familia ya shujaa huyo.

Miongoni mwa watu waliohudhuria mazishi yake ni naibu kiongozi wa mrengo wa Azimio-One Kenya, Bi Martha Karua, mbunge wa zamani wa eneo hilo James Nakhwanga na aliyekuwa mbunge wa Westlands, Fred Gumo (ambaye pia alikuwa waziri).

Waliohutubu katika mazishi yake walimtaja Mzee Mahanga kuwa mtu shujaa, mtumishi aliyejitolea kuhudumia raia na Mkenya mzalendo.

Ingawa vita vya Mau Mau vilikuwa vikiendelea sana katika eneo la Mlima Kenya, Wakenya katika sehemu nyingine nchini walichangia sana juhudi zilizofanya Kenya kujitawala mwaka wa 1962. Kwa mfano, Mzee Mahanga alikuwa mwekahazina wa muungano wa Kavirondo, uliokita shughuli zake katika maeneo ya Nyanza na Magharibi.

Muungano huo ulikuwa miongoni mwa mingine michache Iliyoshirikiana kwa karibu na wapiganaji wa Mau Mau.

Akiwa na umri wa miaka 27 pekee, Mahanga alikamatwa mnamo Aprili 19,

1954 kwa kusaidia wapiganaji. Alikuwa akikusanya pesa ambazo zilitumika kutengeneza bunduki nyumbani kuwapelekea chakula wapiganaji wa Mau Mau.



Aliyekuwa Chifu Mkuu Wanga Mahanga Oniang'

Mahanga alisafirishwa hadi Nairobi, na kuwekwa kizuizini kwa miezi mitatu katika Kambi ya Wafungwa ya Embakasi. Baadaye alipelekwa katika Kambi Maalumu ya Wafungwa, eneo la Lamu.

Katika eneo la Busia, msafara wa magari kadhaa kutoka Kisumu (wakati huo ikiitwa Port Florence) ulifika nyumbani kwake katika kijiji cha Khulwanyange.

Naibu Chifu wa eneo hilo wakati huo, Ismaili Omojo, aliongoza maafisa wa serikali ya kikoloni kufanya msako nyumbani kwa baba yake Mahanga, Mzee David Oniang', kwa kushuku kuwa alikuwaameficha bunduki na silaha nyingine nyumbani kwake.

Operesheni hiyo ilikuwa ya kipekee, kwani wanakijiji walikusanyika kujjonea magari na silaha nzito za kijeshi - lisilo la kawaida katika kijiji chao.

Siku kadhaa n ahata wiki baada ya maafisa hao kuondoka, watu kutoka maeneo maeneobunge ya Funyula na Ugenya walifurika nyumbani kwa Mzee Oniang' kutazama alama za magurudumu zilizoachwa na "magari hayo ya kifahari."

Sifa kuhusu "operesheni hiyo ya kipekee" zilitanda kote. Tukio hilo ndilo lilifanya kijiji cha Khulwanyange kuitwa eneo la Mau Mau.

Mnamo 1958, baada ya kuachiliwa kutoka gerezani katika visiwa vya Mageta, Ziwa Victoria, Mahanga alizidisha uhusiano kati ya eneo lake na wapiganaji wa Mau Mau. Alipelekwa gerezani katika kisiwa hicho baada ya kutolewa Lamu.

Wenyeji wanasema eneo hilo lilitumiwa sana na wafungwa waliokuwa wakitoroka gereza la Mageta. Wafungwa wengi walitoka eneo la Mlima Kenya.

Mahanga aliamua kuishi katika Kata ya Bunyala, alikoanza maisha mapya na wake zake, Bi Wilgada Odinda na Bi Susan Nabwire na wakapata watoto 13.

Kutokana na umaarufu wake, alichaguliwa mbunge wa eneo la Budalang'i mnamo Mei 25, 1963. Huo ndio ulikuwa uchaguzi wa kwanza mkuu nchini.

Mwaka uliofuata, aliteuliwa kuwa Chifu wa Kata ya Bunyala. Alipanda ngazi hadi kuwa Chifu wa Daraja la Juu mnamo 1977. Alihudumu katika kaunti nzima ya Busia (wakati huo ikiwa wilaya) hadi mwaka wa 1981.

Kutokana na utendakazi wake bora, Mahanga alipewa tuzo ya serikali ya Head of State Commendation (HSC) na aliyekuwa wakati huo Rais Daniel Moi kwenye hafla ya kufana iliyofanywa katika Ikulu ya Nairobi mnamo Oktoba 22, 1980.

Akihudumu kama Waziri wa Sheria na Masuala ya Kikatiba katika serikali ya Rais Mwai Kibaki, Bi Karua pia alikutana na Mzee Mahanga na kutambua mchango wake mkubwa katika harakati za kupigania uhuru.

Bi Karua ndiye aliyepokea na kutayarisha kesi ya Mzee Mahanga dhidi ya serikali ya Uingereza, kutokana na mateso ya wapiganaji wa Mau Mau.

Marehemu alisomea katika Shule ya Msingi ya Osieko. Baadaye, alisomea katika shule za Eldoret Union na Kolanya mtawalia kwa Kiwango cha Kawaida (O-Level) na Kiwango cha Juu (A-Level).

Alimaliza masomo yake mnamo 1941. Baadaye, alisomea kozi ya utawala wa umma katika Taasisi ya Mafunzo ya Serikali ya Maseno.

Kutokana na utendakazi wake bora, alikuwa akialikwa kuhudumu kwenye bodi za taasisi tofauti.

Mara kwa mara, alikuwa akihutubia wananchi wakati wa sherehe za sikukuu za kitaifa eneo la Budalang'i na makao makuu ya Kaunti ya Busia.

Kisadfa, wanawe wawili wamefuata nyayo zake. Bw David Mahanga, anayehudumu kama Mshirikishi wa Miradi katika shirika la World Vision, amewahi kuwa diwani wa eneo hilo.

Nduguye, Taabu Mahanga, ni Afisa Mkuu Mtendaji wa chama cha Narc-Kenya. Kupitia kwao, Mzee Mahanga ataendelea kukumbukwa.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

KENYA TOP 100 MID-SIZED COMPANIES
Business Daily KPMG

# EVOLVE

## BECAUSE YOUR BUSINESS DOESN'T STAND STILL – IT EVOLVES

Each stage of your business cycle presents its own set of opportunities and challenges. Do you have what it takes to be successful at each stage? Enter the 2022 Top100 Midsized Companies Survey and take your seat among the great.

**Benefits:**

- Recognition for companies that have successfully redefined their business and remained agile in an increasingly uncertain business landscape.
- Access to an industry benchmarking report and thought leadership to all participating companies.
- Opportunities to network with peers and sponsors through the exclusive Top100 Mid-Sized Companies conference and gala dinner.
- Winners will be eligible to use the 2022 Kenya Top100 Mid-Sized Companies Club logo.

Survey closes on 9 September 2022


**Submit your entry at: www.eastafricatop100.com**

**Kenya100@kpmg.co.ke**

**020 280 6000**







**Be seated among the great.**

Business Daily KPMG

In partnership with:

IFC International Finance Corporation WORLD BANK GROUP
*Creating Markets, Creating Opportunities*

#Top100KE Top100SME @Top100SME

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep




**SMS the word GAZETI to 20567,**
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE SMS text and FREE Delivery**

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*